

MUUNDO WA KIRAI NOMINO KATIKA LAHAJA YA KIMAKUNDUCHI

ASHA IDDI BAVUAI

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA
MASHARTI YA SHAHADA YA UMAHIRI YA KISWAHILI**

(M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2017

UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii yenyе kichwa:

Muundo wa Kirai Nomino katika lahaja ya Kimakunduchi, na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili kukamilisha sehemu ya masharti ya Shahada ya M. A. (Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Dkt. P. P. Lipembe

(Msimamizi)

Tarehe

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile kieletroniki, kurudufu nakala, kurekodi au kwa njia yoyote nyengine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

TAMKO

Mimi **Asha Iddi Bavuai** nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya kutunukiwa shahada ya M.A (Kiswahili) au shahada nyingine yoyote.

.....

Asha Iddi Bavuai

Tarehe.....

TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa wazazi wangu wapendwa, marehemu mama yangu kipenzi **Bi. Zuweina Slim Gharib**, Mwenyezi Mungu amrehemu, amlaze mahala pema peponi **AMIN** na baba yangu **Bw. Iddi Bavuai Iddi**, kwa busara na upendo wao wa kunipa malezi bora na kunipeleka skuli kupata elimu ya dini na dunia ambayo ndio iliyoniongoza katika njia ya kheri.

SHUKURANI

Awali ya yote mwanzo kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu mwingi rehema na mwenye kurehemu kwa kunijaalia afya njema, nguvu na ustahamilivu katika kipindi chote cha masomo yangu mpaka kufanikisha kazi hii. Hivyo basi nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wale wote waliotoa michango yao ya hali na mali hadi kumalizika kwa kazi hii. Si rahisi kuwataja wote kwa majina kutokana na wingi wao na ufinyu wa nafasi bali nachukua fursa hii adhimu kuwashukuru na Mwenyezi Mungu awabariki “**AMIN**”.

Pili, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa msimamizi wangu wa utafiti, Dkt. Peter Lipembe. Shukurani hizo zinaanza pale alipokubali kuwa msimamizi wa kazi hii ya kitaaluma, kisha kwa kuniongoza vyema kwa moyo mkunjufu katika kazi hii ngumu. Kwa kuwa nilikuwa mwanagenzi katika nyanja hii hakuacha kunipa ushauri na maelekezo ambayo kwa njia moja au nyingine yaliboresha kazi hii. Usimamizi wake uliotukuka unanifanya niseme kuwa umenijenga katika fikra za kitaaluma, cha kumlipa sina ila ninamuombea kwa Mwenyezi Mungu amjaalie umri mrefu wenye afya njema ili aweze kurithisha hazina ya elimu aliyonayo kwa wengine wanaoihitaji “**AMIN**”.

Tatu ninatoa shukrani za pekee kutoka moyoni mwangu zimuendee mume wangu mpenzi Bwana Issa Kassim Issa kwa upendo, ushauri na ushirikiano wake ambao ulinifanya niwe na amani katika kipindi chote cha masomo yangu. Mwenyezi Mungu akubariki na akupe umri mrefu wenye afya njema “**AMIN**”.

Nne, ninatoa shukurani za dhati kwa wazazi wangu mama, Zuweina Slim Gharib Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi “AMIN” na baba, Iddi Bavuai Iddi kwa kunilea katika malezi mema na yenye upendo. Pia, ninapenda kuwashukuru wanangu Yahya, Zuweina, Kassim, Amrana na Twahir pamoja na ndugu zangu wependwa kwa mashirikiano yao ya dhati katika kipindi chote cha masomo. Nawaombea Mwenyezi Mungu awabariki na awape afya njema. “AMIN”

Tano, ninawashukuru watoa taarifa wangu wote walioniwezesha kupata data za utafiti huu. Kwa wale niliowapatia hojaji kwa ajili ya kutoa taarifa za utafiti huu waliweza kutumia muda wao ili kuweza kujibu hojaji hizo. Na wale niliowarekodi kwa kinasa sauti walikubali kutumia muda wao kushiriki katika kazi hiyo ya kunipatia data. Sina cha kuwalipa ila taarifa zao walizozitoa ndio zao la utafiti huu wa kitaaluma.

Mwisho, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa wanafunzi wenzangu wa shahada ya uzamili wa Kiswahili wa mwaka 2015/2016 kwa ushirikiano walionipa muda wote wa masomo. Pia ninapenda kuwashukuru wahadhiri wangu wote kwa kunipa ushauri wa kitaaluma na kunitia moyo pale nilipoonekana kukata tamaa. Sina cha kuwalipa ila daima mtakuwa katika kumbukumbu zangu. Mwenyezi Mungu awazidishie moyo wa kupendana na kusaidiana katika raha na shida “AMIN”.

IKISIRI

Utafiti huu umechunguza muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi. Malengo ya utafiti yalikuwa ni kubainisha vipengele vya muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi; kuelezea utaratibu au mpangilio wa vipengele vya muundo wa kirai nomino na lengo la tatu; ni kujadili dhima za kisarufi za kirai nomino. Utafiti huu ultumia mkabala wa kimaelezo katika kukusanya na kuchambua data, huku nadharia ya sarufi miundo virai na dhana yake maarufu ya eksibaa ikiongoza utafiti huu. Utafiti ulifanyika Makunduchi mkoa wa kusini Unguja na ulihusisha shehia tatu ambazo ni shehia ya Kiongoni, shehia ya Nganani na shehia ya Mzuri. Watafitiwa walikuwa ni wazungumzaji asilia wa lahaja ya Kimakunduchi. Watafitiwa hao walichaguliwa kwa kutumia usampulishaji kusudio ambao mtafiti anachagua sampuli kulingana na malengo maalumu. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia njia ya hojaji na uchunguzi makini kuitia shughuli za kijamii kwa mfano mwaka kogwa, sherehe za harusi, maziko na kadhalika. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kutumia mkabala stahilifu ambao ni ule unaotumia maelezo kulingana na data zilizopatikana kutoka kwa watafitiwa. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya sarufi miundo virai na dhana yake maarufu ya eksibaa. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi una sifa za kimuundo ambazo hazipo mbali na lahaja nyingine pamoja na Kiswahili sanifu. Vile vile muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi umeonekana kuwa sawa na ule wa lugha za Kibantu na lahaja za Kiswahili kama ilivyoonyeshwa na wataalamu tofauti.

YALIYOMO

<u>UTHIBITISHO</u>	ii
<u>HAKIMILIKI</u>	iii
<u>TAMKO</u>	iv
<u>TABARUKU</u>	v
<u>SHUKURANI</u>	vi
<u>IKISIRI</u>	viii
<u>YALIYOMO</u>	ix
<u>ORODHA YA MAJEDWALI</u>	xiii
<u>ORODHA YA ALAMA NA VIFUPISHO.</u>	xv
<u>SURA YA KWANZA</u>	1
<u>UTANGULIZI NA USULI WA UTAFITI</u>	1
1.1 <u>Utangulizi</u>	1
1.2 <u>Usuli wa Tatizo la Utafiti</u>	2
1.3 <u>Tatizo la Utafiti</u>	6
1.4 <u>Malengo ya Utafiti</u>	7
1.4.1 <u>Lengo Kuu</u>	7
1.4.2 <u>Malengo Mahususi</u>	7
1.5 <u>Maswali ya Utafiti</u>	7
1.6 <u>Umuhimu wa Utafiti</u>	7
1.7 <u>Mipaka ya utafiti</u>	8
1.8 <u>Hitimisho</u>	8
<u>SURA YA PILI</u>	9

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA	9
<u>2.1 Utangulizi</u>	9
<u>2.2 Mapitio kuhusu Nadharia ya Kirai Nomino</u>	9
<u>2.2.1 Maana ya Kirai Nomino</u>	9
<u>2.2.2 Muundo wa Virai Nomino kwa Jumla</u>	10
<u>2.2.3 Muundo wa Virai katika Kiswahili</u>	11
<u>2.2.4 Dhima za Kisarufi za Kirai Nomino</u>	16
<u>2.3 Tafiti Tangulizi kuhusu Virai-Nomino</u>	18
<u>2.4 Kiunzi cha Nadharia</u>	31
<u>2.4.1 Nadharia ya Eksibaa</u>	31
<u>2.5 Hitimisho</u>	36
SURA YA TATU	37
MBINU ZA UTAFITI	37
<u>3.1 Utangulizi</u>	37
<u>3.2 Mkabala wa Utafiti</u>	37
<u>3.3 Eneo la Utafiti</u>	37
<u>3.4 Kundu Lengwa</u>	38
<u>3.5 Sampuli na Usampulishaji</u>	38
<u>3.5.1 Sampuli.</u>	38
<u>3.5.2 Mchakato wa Usampulishaji.</u>	38
<u>3.6 Mbinu za Ukusanyaji Data</u>	39
<u>3.6.1 Uchunguzi makini</u>	40
<u>3.6.2 Hojaji</u>	40

<u>3.7 Mkabala wa Kimaadili ya Utafiti</u>	41
<u>3.8 Uchanganuzi wa Data</u>	42
<u>3.9 Vifaa vya Utafiti</u>	42
<u>3.10 Hitimisho</u>	43
<u>SURA YA NNE</u>	44
<u>UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI</u>	44
<u>4.1 Utangulizi</u>	44
<u>4.2 Muundo wa Virai Nomino katika Lahaja ya Kimakunduchi</u>	44
<u>4.2.1 Kirai Nomino cha Muundo wa Nomino moja Pekee (N)</u>	44
<u>4.2.2 Kirai Nomino Cha Nomino na Kivumishi (N + V)</u>	46
<u>4.2.3 Kirai Nomino cha Kiwakilishi Pekee (W)</u>	47
<u>4.2.4 Kirai Nomino cha Nomino na Kishazi Tegemezi (N + Kish - teg)</u>	48
<u>4.2.5 Kirai Nomino chenye Muundo wa Kitenzi Jina (TJ)</u>	49
<u>4.2.6 Kirai Nomino cha Muundo wa Kitenzi Jina na Kivumishi (TJ+ V)</u>	50
<u>4.2.7 Kirai Nomino cha Muundo wa Nomino, Kivumishi na Kishazi Tegemezi</u>	51
<u>4.2.8 Kirai Nomino cha Muundo wa Kiwakilishi na Kivumishi (W+V)</u>	53
<u>4.3 Kuchanganua Utaratibu au Mpangilio wa Vipengele katika Kirai Nomino</u>	54
<u>4.3.1 Kirai Nomino chenye Nomino, Vivumishi na Kishazi Tegemezi (N+V+Kish-teg)</u>	55
<u>4.3.2 Kirai Nomino cha Kiwakilishi na Vivumishi (W + V)</u>	57
<u>4.3.3 Kirai Nomino cha Nomino, Kitenzi Jina na Kivumishi (TJ+ V)</u>	58
<u>4.4 Kubainisha Dhima za Kisarufi za Kirai Nomino katika Lahaja ya Kimakunduchi</u>	62

<u>4.4.1 Dhima ya Kubainisha Kiima katika Tungo</u>	62
<u>4.4.2 Dhima ya kuwa Yambwa Tendwa (Kipozi)</u>	64
<u>4.4.3 Dhima ya kuwa Yambwa Tendewa (Kitondo)</u>	66
<u>4.4.4 Dhima ya kuwa Kijalizo cha Kiima</u>	67
<u>4.4.5 Dhima ya kuwa Kijalizo cha Kivumishi</u>	69
<u>4.4.6 Dhima ya kuwa Kijalizo cha Kihusishi</u>	71
<u>4.5 Hitimisho</u>	75
<u>SURA YA TANO</u>	76
<u>MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI</u>	76
<u>5.1 Utangulizi</u>	76
<u>5.2 Muhtasari wa Utafiti</u>	76
<u>5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti</u>	77
<u>5.4 Mapendekezo</u>	78
<u>5.4.1 Mapendekezo ya Jumla</u>	78
<u>5.4.2 Tafiti Fuatishi</u>	79
<u>5.5 Hitimisho</u>	80
<u>MAREJEO</u>	81
<u>VIAMBATANISHO</u>	86

ORODHA YA MAJEDWALI

<u>Jedwali Na. 2. 1 Mpangilio wa Viandami katika baadhi ya Lugha za Kibantu.</u>	24
<u>Jedwali Na. 2.2 Nafasi ya kivumishi</u>	26
<u>Jedwali Na. 2.4 Nafasi ya Kibainishi ‘kila’ katika Lugha Tofauti.</u>	27
<u>Jedwali Na. 4.1 Kirai Nomino cha Muundo wa Nomino moja Pekee (N)</u>	45
<u>Jedwali Na. 4.2 Kirai Nomino Cha Nomino na Kivumishi (N + V)</u>	46
<u>Jedwali Na. 4.3 Kirai Nomino cha Kiwakilishi Pekee (W)</u>	47
<u>Jedwali Na. 4.4 Kirai Nomino cha Nomino na Kishazi Tegemezi (N + Kish - teg)</u>	48
<u>Jedwali Na. 4.5 Kirai Nomino chenye Muundo wa Kitenzi Jina (TJ)</u>	49
<u>Jedwali Na. 4.6 Kirai Nomino cha Muundo wa Kitenzi Jina na Kivumishi (TJ+ V)</u>	50
<u>Jedwali Na. 4.7 Kirai Nomino cha Muundo wa Nomino, Kivumishi na Kishazi Tegemezi Kivumishi (N + V + Kish-teg - V)</u>	51
<u>Jedwali Na. 4.8 Kirai Nomino cha Muundo wa Kiwakilishi na Kivumishi (W+V)</u>	53
<u>Jedwali Na. 4.9 Vipashio vya Muundo wa Kirai Nomino</u>	54
<u>Jedwali 4.10 Kirai Nomino chenye Nomino, Vivumishi na Kishazi Tegemezi (N+V+Kish-teg)</u>	55
<u>Jedwali 4.11 Kirai Nomino cha Kiwakilishi na Vivumishi (W + V)</u>	57
<u>Jedwali 4.12 Kirai Nomino cha Nomino, Kitenzi Jinan a Kivumishi (TJ+V)</u>	58
<u>Jadweli Na. 4.13 Muhtasari wa Vipengele vya Muundo wa Kirai Nomino cha Kimakunduchi.</u>	61
<u>Jadweli Na. 4.14 Kutanuka kwa Vikundi Nomino</u>	61
<u>Jadweli Na. 4.15 Dhima ya kubainisha Kiima katika Tungo</u>	63
<u>Jadweli Na. 4.16 Dhima ya kuwa Yambwa Tendwa (Kipozi)</u>	65

<u>Jadweli Na. 4.17 Dhima ya kuwa Yambwa Tendewa (Kitondo)</u>	66
<u>Jadweli Na. 4.18 Dhima ya kuwa Kijalizo cha Kiima</u>	68
<u>Jadweli Na. 4.19 Dhima ya kuwa Kijalizo cha Kivumishi</u>	70
<u>Jadweli Na. 4.20 Dhima ya kuwa Kijalizo cha Kihusishi</u>	72

ORODHA YA ALAMA NA VIFUPISHO.

/	Au
	Inawakilisha
B	Kibainishi
H	Kihisishi
K	Kiima
KH	Kirai kihisishi
Kish-teg	Kishazi tegemezi
Kish-teg-V	Kishazi tegemezi kivumishi
KN	Kirai nomino
KT	Kirai kitenzi
KV	Kirai kivumishi
N	Nomino
Na	Namba
S	Sentensi
T	Kitenzi kikuu
t	Kitenzi kishirikishi
TJ	Kitenzi jina
Ts	Kitenzi kisaidizi
V	Kivumishi
VN	Virai Nomino
W	Kiwakilishi

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI NA USULI WA UTAFITI

1.1 Utangulizi

Uchunguzi wa kirai nomino katika lugha za Kibantu ni moja ya maeneo ya utafiti ambayo yameshughulikiwa katika miaka ya karibu. Watafiti wengi wa lugha hizo wamevutika sana kufanya tafiti kuhusiana na muundo wa kirai nomino, kwani kipengele hiki cha isimu ni muhimu sana katika muundo na maana ya lugha yoyote ile iwayo. Umuhimu wa kipengele hiki unatokana na ukweli kuwa kinabeba nomino, ambayo ni kipengele msingi cha kimuundo kinachobeba dhima kubwa katika kukamilisha maana ya usemi (sentensi). Katika lugha ya Kiswahili nomino ni kipengele muhimu sana cha muundo na maana katika sentensi za lugha hii; kama Mbaabu (1985) anasisitiza kuwa ; Majina (nomino) ya Kiswahili ni muhimu sana hivi kwamba muundo wa maneno mengine katika sentensi hutegemea majina muhimu ya sentensi. Hapa anamaanisha kwamba, nomino ndilo neno linalotawala maneno mengine katika sentensi na kuathiri muundo wa maneno haya.

Kwa upande mwengine umuhimu wa Kirai Nomino katika lugha ultambulika na Waasisi wa Sayansi wa Ulaya wakati mada hii ilipofanywa kuwa ndio dhamira kuu katika mradi wao ulioitwa Eurotyp Project (*Programme in Language Typology*, 1990-4; Siewierska, 1997). Mradi huu ulishughulikia lugha kuu zilizopo Ulaya, na sio kuangalia lugha ya Kiingereza peke yake tu. Kinadharia, pamoja na tafiti zilizofanywa juu ya virai nomino vya Kibantu, sehemu walizokuwa wakivutika nazo

ni uchambuzi wa lugha hizo. Kwa mfano, Kijakazi (2012) amebainisha virai nomino katika lahaja ya Kitumbatu, Magashi (2008) amechunguza miundo ya virai nomino vyta Kisukuma, Ndomba (2006) naye aliandika juu ya muundo wa virai nomino katika Kisamatego, na Neekamiah (2010) aliandika juu ya muundo wa virai nomino katika Kihangaza. Tafiti hizi zina thamani kubwa sana lakini kwa bahati mbaya hakuna kazi yoyote iliyofanywa ambayo imeshughulikia kwa ukamilifu juu ya muundo wa kirai nomino na kuangalia kiundani utaratibu / mpangilio wa vipengele katika kirai nomino cha Kiswahili cha Kimakunduchi. Kwa hivyo utafiti huu una lengo la kusawazisha mapungufu hayo pamoja na kuchunguza dhima za kisarufi za virai hivyo katika lahaja ya Kimakunduchi.

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Wataalamu mbalimbali wamejadili dhana ya kirai. Miongoni mwao ni Culicover (1976), Massamba (2004), Longhorn (2011), na Radford (2004). Massamba (2004) ameleezea kirai kuwa ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja na hakina uhusiano wa kiima-kiarifu (yaani hakihuishi mtendaji wa tendo na tendo lililotendwa). Ameeleeza zaidi kwa kusema kuwa uhusiano wa kiima-kiarifu ni hali ya tungo inayoonyesha kuwapo kwa tendo na mtendaji wa tendo. Kirai kwa kawaida, huweza kuundwa na neno kuu peke yake au na neno likiambatana na neno au maneno mengine kutokana na mahusiano maalumu yaliyokitwa katika tabia za asili za neno kuu.

Radford (2004), anadai kuwa kila kirai kina kichwa kinachoamua sifa za kirai chote.

Kwa mfano

Mwanafunzi wa hisabati.

K

Mwanafunzi (umoja) ni kichwa cha kirai na ndicho kinachoamua sifa za kirai husika. Kirai huainishwa kimuundo kulingana na neno kuu/ kichwa cha kirai husika. Kwa mfano: Kirai ambacho neno lake kuu ni nomino/ au kiwakilishi huitwa kirai nomino, kwa mfano:

Mtoto huyu. Hapa neno kuu ni mtoto ndipo kirai hicho kikaitwa kirai nomino.

Pia Longhorn (2011) anadai kuwa kirai ni kipashio cha kisarufi kinachoundwa na neno moja au zaidi na hakina mwingiliano wa kimuundo wa kiima - kiarifu. Culicover (1976) anadai kuwa kirai ni mfuatano wowote wa maneno katika lugha yoyote na maneno yenye ni ya kategoria fulani. Kuna mfuatano wa maneno ulio mfupi kuliko sentensi lakini ni ndefu kuliko neno moja. Kwa hiyo kuna virai vilivyo virefu kuliko neno moja lakini vifupi kuliko sentensi.

Kwa kuwa katika mfumo wa lugha huwa kuna aina mbalimbali za maneno basi pia kuna aina mbalimbali za virai, kama vile virai nomino, virai vitenzi, virai vivumishi, virai vielezi na kadhalika. Katika utafiti huu tutachunguza muundo wa virai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi.

Kirai nomino ni kipashio cha kiisimu kilichojadiliwa sana katika lugha za Kibantu na lahaja za Kiswahili (Rugemalira, 2007 ; Neekemiah, 2010 ; Ndomba, 2006 ;

Masebo na Nyangwine, 2007 ; Kadege, (2009) ; Radford, 2004 ; OXFORD, 2011 ; Riro, 2012 na Massamba na wenzake, 2009). Kadege (2009) anasema kirai nomino ni kirai ambacho neno lake kuu ni nomino. Oxford (2011) ameeleza kuwa kirai nomino ni kirai ambacho neno lake kuu linalotawala ni nomino. Neno hili huweza kusimama peke yake au kuambatana na maneno mengine mbalimbali. Kwa mfano;

Samaki ni chakula bora.

K

Radford (2004) ameeleza kuwa kirai nomino ni aina ya kirai ambacho hufanya kazi kama nomino. Neno kuu la kirai nomino ni nomino au kiwakilishi cha nomino. Pia, Masebo na Nyangwine (2007) wamefasili kirai nomino kuwa ni kirai ambacho muundo wake umekitwa kwenye nomino au mahusiano ya nomino na neno au mafungu ya maneno. Kwa upande mwengine Riro (2012) ameeleza kuwa kirai nomino hujengwa kwa nomino moja au zaidi au viwakilishi vya nomino. Kirai hapa hudokeza taarifa inayohusu nomino au kiwakilishi cha nomino.

Kwa upande wa miundo ya virai nomino wataalamu wametofautiana wako wanaosema kuna miundo minane (8), kwa mfano Oxford (2011) ameainisha kama hivi ifuatavyo; nomino moja, nomino mbili au zaidi, kiwakilishi, nomino na kivumishi, kitenzi jina, nomino na kishazi tegemezi kivumishi, kivumishi na nomino, na kiwakilishi na kivumishi. Kwa upande wa Riro (2012) ameainisha miundo tisa (9), minane (8) kama aliyolezea Oxford na wa tisa ni; nomino na kitenzi jina na kivumishi. Masebo na Nyangwine (2007) wao wameainisha miundo tisa, minane

sawa sawa na wenzake na wa tisa ni; nomino na kirai kivumishi. Radford (2004) ameainisha miundo mitano (5) nayo ni; nomino (kiwakilishi) na kivumishi, kivumishi na nomino (kiwakilishi), nomino ya kitensi jina na kivumishi, nomino (kiwakilishi) na nomino (kiwakilishi) na ya tano ni nomino (kiwakilishi) na kirai kihusishi. Pia ameeleza kuwa kirai nomino katika sentensi za Kiswahili huwa na majukumu mbalimbali kisintaksia. Majukumu hayo ni:

(i) Kiima

Kiima ni sehemu ya sentensi ambayo hutuambia ni nani / nini kinachozungumziwa katika sentensi. Kwa mfano:

Mkuu wa shule amenipa kazi nyingi.

K

(ii) Yambwa tendwa.

Yambwa tendwa (kipozi) ni nomino ambayo huathiriwa na tendo moja kwa moja. Ni kijalizo cha kitensi. Kwa mfano: Mama hupika wali.

Oxford (2011) ameeleza kuwa kirai nomino hutekeleza dhima mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Dhima hizo ni pamoja na:

- a) Kuunda tungo, yaani tungo ya kirai nomino. Kwa mfano: mkate mkavu, nyumba yangu ndogo n.k.
- b) Kubainisha mtenda. Kwa mfano: Mwalimu wetu alitutungia zoezi.
- c) Kuwa shamirisho. Kwa mfano: Kadogoo ni mtoto mpole. .

Kutokana na watafiti waliofanya tafiti kuhusu muundo wa kirai nomino wengi wao wamechunguza kupitia lugha za Kibantu na wachache katika lahaja za Kiswahili, miongoni mwao ni Kijakazi (2012) amechunguza muundo wa virai nomino katika lahaja ya Kitumbatu, Magashi (2008) amechunguza muundo wa virai nomino vya Kisukuma. Ndomba (2006) naye aliandika juu ya muundo wa virai nomino katika Kisamatego, pia Neekamiah (2010) aliandika juu ya muundo wa virai nomino katika Kihangaza.

Kwa uelewa wa mtafiti bado hajaona utafiti wowote uliochunguza muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi. Hali hiyo, imeacha pengo kubwa kwa jamii na kupelekea baadhi ya watu kufanya makosa katika matumizi ya muundo wa kirai nomino katika lahaja hiyo. Kwa hiyo mtafiti ameona kuna haja ya kuchunguza muundo wa virai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi.

1.3 Tatizo la Utafiti

Lahaja ya Kimakunduchi ni moja ya lahaja kuu za Kiswahili, hata hivyo ni tafiti chache sana zimefanywa kuhusu vipengele mbalimbali vya isimu ya lahaja hii. Hii ina maana kwamba taaluma zake nyingi hazipo katika maandiko. Hili ni tatizo kubwa la kwanza ambalo utafiti huu ulijielekeza katika kulitatua. Madhumuni ya utafiti huu ni kuchunguza muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi, na pia kubainisha mpangilio au utaratibu wa mfuatano wa vipengele hivyo katika lahaja hii.

Kwa upande mwingine, kutokana na kutofanyiwa uchunguzi mpana wa lahaja hii, hakuna taarifa zozote kuhusu vipengele vyake vingi vya kiisimu. Hivyo kazi hii ilijielekeza katika kukabili kwa undani kipengele chake kimoja wapo cha kiisimu ambacho ni muundo wa virai nomino vyake. Kuhusiana na lahaja ya Kimakunduchi, tatizo la utafiti huu ni kuelezea kwa undani kipengele cha muundo wa kirai nomino katika lahaja hii ili kubainisha vipashio vinavyoandamana na nomino katika kuunda kirai nomino, vilevile umebainisha mpangilio au utaratibu wa mfuatano wa vipengele hivyo katika kujenga kirai nomino.

1.4 Malengo ya Utafiti

1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi. Katika kufikia lengo hili, utafiti uliongozwa na malengo mahususi yafuatayo ;

1.4.2 Malengo Mahususi

- 1) Kubainisha vipengele vya muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi.
- 2) Kuelezea utaratibu / mpangilio wa vipengele vya muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi.
- 3) Kujadili dhima za kisarufi za kirai nomino cha lahaja ya Kimakunduchi.

1.5 Maswali ya Utafiti

- 1) Muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi una vipengele vipi?
- 2) Vipengele vya kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi vipo katika mpangilio upi?
- 3) Kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi kina dhima gani za kisarufi?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Mtafiti yeoyote wa kitaaluma huwa na shauku ya kuongeza maarifa yenye kuleta tofauti na kuongeza ufanisi katika uwanja anaoutafiti. Utafiti huu kuhusu muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi una umuhimu ufuatao; kwanza, utasaidia kuhifadhi lahaja ya Kimakunduchi kimaandishi. Pili, utasaidia kuziba pengo la kutofanyiwa utafiti kwa vipengele vya kiisimu vya lahaja ya Kimakunduchi kuliko lahaja nyengine zilizopo upwa wa Afrika Mashariki. Tatu, utafiti huu utasaidia kuwa marejeleo kwa watafiti wengine ambao wana kusudia kutafiti lahaja mbalimbali za mwambao wa Afrika Mashariki.

1.7 Mipaka ya utafiti

Utafiti huu umeshughulikia kuchanganua muundo wa virai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi, kubainisha vipengele vya muundo huo pamoja na kuchanganua utaratibu / mpangilio wa vipengele katika kirai nomino. Pia kubainisha dhima za kisarufi za kirai nomino.

1.8 Hitimisho

Sura hii imejadili taarifa mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti ambayo ni “Muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi”. Maeleo yameanza kwa kuelezea utangulizi na usuli wa mada ya utafiti. Sura hii pia imeonyesha tatizo la utafiti. Vilevile imebainisha malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti pamoja na mipaka ya utafiti

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii imejadili kazi tangulizi mbalimbali zinazohusiana na mada ya kirai nomino. Vilevile imeelezea kiunzi cha nadharia kilichotumika katika utafiti huu. Uchambuzi wa kazi tangulizi ambao umegawika katika sehemu mbili; ya kwanza inahusu mapitio kuhusu nadharia ya kirai nomino, na sehemu ya pili inahusu mapitio ya tafiti zilizofanywa katika lugha mbalimbali kuhusu kirai nomino.

2.2 Mapitio kuhusu Nadharia ya Kirai Nomino

2.2.1 Maana ya Kirai Nomino

Dhana ya maana ya kirai nomino kama kipashio cha kiisimu imejadiliwa sana na wataalamu waliochunguza lugha mbalimbali hususani lugha za Kibantu na lahaja za Kiswahili (Radford, 2004 ; Rugemalira, 2007 ; Neekemiah, 2010 ; Ndomba, 2006 ; Masebo na Nyangwine, 2007 ; Kadege, 2009 ; Oxford, 2011 ; Riro, 2012 na Massamba na wenzake, 2009).

Kwa maelezo ya Radford (2004) ameeleza kuwa kirai nomino ni aina ya kirai ambacho hufanya kazi kama nomino. Neno kuu la kirai nomino ni nomino au kiwakilishi cha nomino. Hujengwa na nomino, viwakilishi pekee au pamoja na maneno mengine yanayohusiana na nomino au viwakilishi hivyo.

Mtazamo huu unashikiliwa pia na Kadege (2009) ameeleza kuwa kirai nomino ni kirai ambacho neno lake kuu ni nomino.

Kwa upande mwingine, Oxford (2011) ameelleza kuwa kirai nomino ni kirai ambacho neno lake kuu linalotawala ni nomino. Neno hili huweza kusimama peke yake au kuambatana na maneno mengine mbalimbali. Kwa mfano; **Samaki** ni chakula bora.

Masebo na Nyangwine (2007) nao wamefasili kirai nomino kuwa ni kirai ambacho muundo wake umekitwa kwenye nomino au mahusiano ya nomino na neno au mafungu ya maneno.

Riro (2012) ameelleza kuwa kirai nomino hujengwa kwa nomino moja au zaidi au viwakilishi vya nomino. Kirai hapa hudokeza taarifa inayohusu nomino au kiwakilishi cha nomino. Kutokana na uchambuzi wa kazi za wataalamu hawa, dhana ya jumla inayopatikana kuhusu maana ya kirai nomino ni kuwa kirai nomino ni kirai ambacho neno lake kuu ni nomino au kiwakilishi cha nomino na huweza kusimama peke yake au kuambatana na maneno mengine.

2.2.2 Muundo wa Virai Nomino kwa Jumla

Kwa upande wa miundo ya virai nomino, uchambuzi wa wataalamu umetofautiana ; wako wanaosema kuna miundo minane (8) ya kirai nomino ; kwa mfano Oxford (2011) ameainisha aina zifuatazo za kirai nomino; Nomino moja, nomino mbili au zaidi, kiwakilishi, nomino na kivumishi, kitenzi jina, nomino na kishazi tegemezi

kivumishi, kivumishi na nomino, na kiwakilishi na kivumishi. Kwa upande mwingine, Riro (2012) ameainisha miundo tisa (9), minane (8) kama aliyoielezea Oxford na wa tisa ni; nomino na kitenzi jina na kivumishi. Masebo na Nyangwine (2007) nao wameainisha kirai nomino katika miundo tisa, minane sawa sawa na wenzake na wa tisa ni; nomino na kirai kivumishi.

Naye Radford (2004) ameainisha miundo mitano (5) ya kirai nomino, nayo ni; nomino (kiwakilishi) na kivumishi, kivumishi na nomino (kiwakilishi), nomino ya kitenzi jina na kivumishi, nomino (kiwakilishi) na nomino (kiwakilishi) na ya tano ni nomino (kiwakilishi) na kirai kihuishi. Uchambuzi wa wataalamu hawa umemsaidia mtafiti kuweza kubainisha jinsi lugha mbalimbali zinavyodhihirisha miundo tofauti ya kirai nomino.

2.2.3 Muundo wa Virai katika Kiswahili

Katika sehemu iliyotangulia tumeangalia mapitio ya kazi tangulizi zilizoelezea juu ya miundo ya kirai nomino katika lugha mbalimbali. Masamba na wenzake (2009) wamejadili virai katika Kiswahili sanifu kwa kuonesha kwamba kirai huundwa kutokana na mahusiano maalumu baina ya maneno. Mahusiano hayo huwa ni ya asili katika lugha na hujidhihirisha kisarufi. Muundo wa kirai hukitwa katika neno kuu katika lugha kama vile nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi na hata viunganishi. Maneno haya makuu ndiyo hutupatia aina mbali mbali za virai. Kwa mfano, katika Kiswahili kuna aina za virai kama vile: virai nomino, virai vitenzi, virai vielezi, virai vivumishi, virai viunganishi (Khamis 2009). Kwa mfano ;

1) Virai nomino (VN) Mfano:

a) *Mtu mrefu.*

b) *Walimu na wanafunzi* watasafiri kesho.

Katika mifano ya hapo juu mafungu ya maneno yaliyoandikwa kwa herufi mlazo ni mfano wa virai nomino ambavyo vimechunguzwa katika utafiti huu. Aina hii ya virai nomino katika Kimakunduchi imejadiliwa kwa kina katika sura ya nne.

Radford (2004) ameeleza kuwa kirai nomino ni aina ya kirai ambacho hufanya kazi kama nomino. Neno kuu la kirai nomino ni nomino au kiwakilishi cha nomino. Kirai nomino hujengwa na nomino, viwakilishi pekee au pamoja na maneno mengine yanayohusiana na nomino au viwakilishi hivyo. Kirai nomino huweza kuundwa na ;

i. Nomino (kiwakilishi) na kivumishi (N+V), kwa mfano:

Mwalimu mwingine

N + V

ii. Kivumishi na nomino (*kiwakilishi*) (V+N) kwa mfano:

Hawa wanawake

V + N

iii. Nomino ya kitende jina na kivumishi (N+V), kwa mfano:

Kuimba kwao

N + V

iv. Nomino (kiwakilishi) na nomino (kiwakilishi) (N+N), kwa mfano:

Mama na baba.

v. Nomino (kiwakilishi) pamoja na kirai husishi, kwa mfano:

Mtoto wa mwalimu.

Kirai nomino huweza kuwa kiima au yambwa (kitendwa/ kitendewa) au kijalizo katika sentensi. Matei (2008) ameeleza yafuatayo kuhusu kijalizo: kijalizo ni istilahi inayotokana na kitenzi ‘jaliza’ ambacho kina maana ‘kamilisha’/ ‘ongezea’ habari ili kukamilisha au kutosheleza maana. Kijalizo ni neno/ kirai ambacho hufuata kitenzi kishirikishi na ambacho huelezea zaidi kiima au yambwa. Kijalizo huongezea maana/ hukamilisha maana ya kipashio kingine katika sentensi. Kwa mfano;

(a) *Mji huo una wezi wengi.*

Mji huo ni kiima na wezi wengi ni kijalizo

(b) *Sisi sote tulijaribu maswali hayo.*

Katika sentensi (b) sisi sote ni kiima na maswali hayo ni yambwa tendwa kimapokeo lakini huwa ni kijalizo katika nadharia ya Eksibaa.

Masebo na Nyangwine (2007) wameelezea aina tisa za miundo ya virai nomino kama ifuatavyo;

a) Nomino peke yake.Mfano: **Chaki** zimekwisha.

b) Nomino mbili au zaidi zilizounganishwa. Mfano: **Baba na mama** wanalima.

c) Nomino na kivumishi kimoja au zaidi.Mfano: **Mtu mnene** ameanguka.

- d) Vivumishi na jina. Mfano: **Kile kitabu** ni kizuri.
- e) Jina na kishazi tegemezi kivumishi. Mfano: **Mtoto aliyejeka jana** ameondoka.
- f) Nomino, kivumishi na kishazi tegemezi yumishi. Mfano: **Mtoto mzuri uliyemuona jana** ni mwanangu.
- g) Kiwakilishi peke yake Mfano: **Wewe** huna matatizo.
- h) Nomino na kirai yumishi. Mfano: **Mzee mwenye duka kubwa kule kijijini** ameuza kila kitu
- i) Kiwakilishi na kivumishi. Mfano: **Vyake vyote** viuzwe tu.

Mifano ya hapo juu maneno yote ambayo yamekozeshwa ni virai nomino. Oxford (2011) amesema kuwa kuna vipashio vinane vinavyounda virai nomino navyo ni;

- 1) Nomino moja. Mfano: **Mvua** inanyesha.
- 2) Nomino mbili au zaidi. Mfano: Anafuga **kuku na bata**.
- 3) Kiwakilishi. Mfano: Mimi simfahamu.
- 4) Nomino na kivumishi. Mfano: Nimekunywa **chai tamu**.
- 5) Kitenzi jina. Mfano: **Kusoma** kwa bidii kumemsaidia.
- 6) Nomino na kishazi tegemezi kivumishi. Mfano Nitafutie **mtu anayeweza kuimba**.
- 7) Kivumishi na nomino. Mfano: **Hicho chumba** kitapangishwa.
- 8) Kiwakilishi na kivumishi. Mfano: Nipatie **hicho kidogo**

Kwa upande mwengine, Riro (2012) ameeleza kuwa kirai nomino hujengwa kwa nomino moja au zaidi au viwakilishi vya nomino. Kirai hapa hudokeza taarifa inayohusu nomino au kiwakilishi cha nomino. Kirai nomino huweza kuwa na miundo ifuatayo:

- a) *Nomino pekee.* Mfano: Bata wetu amepotea.
- b) *Nomino mbili au zaidi zilizounganishwa na kiunganishi.* Mfano:
Walimu, wazazi na wanafunzi walihudhuria mkutano.
- c) *Nomino na kivumishi kimoja au zaidi.* Mfano: Nyumba kubwa imebomolewa.
- d) *Kivumishi na nomino.* Mfano: Wale wanachuo wamegoma kufanya jaribio.
- e) *Kiwakilishi pekee.* Mfano: Nyinyi mtasafiri kesho jioni.
- f) *Kiwakilishi na kivumishi.* Mfano: Wale wakorofí wamefukuzwa.
- g) *Nomino na kishazi tegemezi.* Mfano: Mwalimu aliyejukua juzi amefariki.
- h) *Nomino, kivumishi na kishazi tegemezi kivumishi.* Mfano: Kamusi kubwa iliyonunuliwa jana imeibiwa.
- i) *Nomino ya kitenzi jina na kivumishi.* Mfano: Kuondoka kwake kumewafurahisha wengi.

Katika mifano ya hapo juu, maneno yaliyopingwa mstari ni virai nomino katika Kiswahili sanifu. Kazi za wataalamu hawa zimemsaidia mtafiti kubainisha vipengele vya muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi.

Fromkin (2000) ameeleza kuwa muundo wa kirai nomino cha Kiingereza ni kama ulivyojitekeza katika mifano hapo chini;

- i. N + KH KN kama **murderer of Dancan** ‘muuaji wa Dancan’
- ii. N KN kama **murderer** ‘muuaji’
- iii. V + KN KN kama **old king of France** ‘mfalme mzee wa Ufaransa’

Hudson (2000) anadai kuwa kanuni ya muundo wa kirai nomino cha Kiingereza ni; KN (B) (KV) N (KH) yaani KN huwa na nomino kama neno kuu linaloweza kutanguliwa na kibainishi na/au kirai kivumishi na likafuatiwa na kirai kihusishi. Vifungu vilivyopo katika mabano vinaweza kujitokeza au visijitokeze.

Ashton (1944) amedai kuwa katika Kiswahili neno kuu hufuatwa na kivumishi ambacho huwa na upatanisho wa kisarufi na nomino. Ameeleza kuwa viandami vingine vya kirai nomino ni vibainishi, vishazi rejeshi na vivumishi vya –enye kama vinavyojitokeza katika mifano ifuatayo hapo chini;

- a) Nyumba hii.
- b) Wagonjwa wale.

2.2.4 Dhima za Kisarufi za Kirai Nomino

Sarufi ni mfumo wa kanuni za lugha zinazomwezesha mzungumzaji kutunga sentensi nyingi, sahihi na zenye kukubaliwa na wazawa wa lugha, Mdee (1999). Kwa hiyo dhima za kisarufi za kirai nomino ni majukumu ya kisarufi ambayo kirai nomino hutekeleza katika kutunga sentensi za lugha ya Kiswahili. Oxford (2011) ameeleza kuwa kirai nomino hutekeleza dhima mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Dhima hizo ni pamoja na:

- a) Kuunda tungo, yaani tungo ya kirai nomino. Kwa mfano: *mkate mkavu, nyumba yangu* ndogo n.k.
- b) Kubainisha mtenda. Kwa mfano: *Mwalimu wetu* alitutungia zoezi.
- c) Kuwa shamirisho. Kwa mfano: *Kadogoo ni mtoto mpole.*

Pia Radford (2004) ameeleza kuwa kirai nomino katika sentensi za Kiswahili huwa na majukumu mbalimbali ya kisintaksia. Majukumu hayo ni pamoja na:

- (i) **Kiima.** Hii ni sehemu ya sentensi ambayo hutuambia ni nani / nini kinachozungumziwa katika sentensi. Kwa mfano: *Mkuu wa shule amenipa kazi nyingi.*
- (ii) **Yambwa tendwa.** Yambwa tendwa (kipozi) ni nomino ambayo huathiriwa na tendo moja kwa moja. Ni kijalizo cha kitenzi. Kwa mfano: *Mama hupika wali.*
- (iii) **Yambwa tendewa (kitondo).** Yambwa tendewa ni nomino inayotaja mtu ambaye anaathiriwa na kitendo kwa njia isiyo ya moja kwa moja (anayefaidika au kuhasirika kutokana na kitendo). Ni kijalizo cha kitenzi. Kwa mfano: *Jamila aliwanunulia watoto wake zawadi.*
- (iv) **Kijalizo cha kiima.** Kijalizo cha kiima ni kijalizo ambacho urejeshi wake ni kwa kiima. Hasa katika sarufi mapokeo. *Kalulu alikuwa daktari mzuri. Uwakilishi wake katika tungo utakuwa kijalizo cha kiima.*

(v) Kijalizo cha kivumishi. Ni kijalizo ambacho kinajaliza kivumishi hasa cha ‘a’ unganifu.

Mfano: *Uongo wa wanasiasa nchini umedhahirika.*

‘Wanasiasa nchini’ ni kirai nomino kinachokamilisha kivumishi ‘wa’.

(vi) Kijalizo cha kihuishi. Kirai nomino hufanya kazi ya kijalizo kinachokamilisha kihuishi kama inavyooneshwa katika mfano ufuatao; *Paka amelala juu ya kitanda changu.* Katika sentensi hii ‘*Kitanda changu*’ ni kirai nomino kinachokamilisha kihuishi ‘juu ya’.

Akmajian na wenzake (2007 :182) wanadai kuwa KN hufanya kazi tofauti kisarufi kulingana na mahali kilipo katika sentensi hata kama sentensi hizo zina miundo inayofanana. Kwa mfano ;

- a) *The people in the room frightened the boy.* ‘watu waliokuwa katika chumba walimuogopesha mvulana’
- b) *The boy frightened the people in the room.* ‘mvulana aliwaogopesha watu waliokuwa katika chumba’

Akmajian (keshatajwa) anadai kuwa katika miundo hiyo hapo juu KN ‘**the people in the room**’ katika (a) hapo juu inafanya kazi ya kiima cha sentensi ambapo kirai hicho hicho katika (b) kinafanya kazi ya yambwa.

Kazi za wataalamu hawa zimemsaidia mtafiti kuweza kubainisha dhima za kisarufi za kirai nomino cha Kimakunduchi.

2.3. Tafiti Tangulizi kuhusu Virai-Nomino

Tafiti mbalimbali zimekwishafanywa kuhusu virai nomino vya lugha mbalimbali. Magashi (2008) alifanya utafiti juu ya miundo ya virai nomino katika Kisukuma. Katika utafiti huu alibainisha kuwa kirai nomino cha Kisukuma kinaweza kubeba vibainishi kuanzia kimoja hadi vinne. Hali hii inategemea nomino inayobainishwa na maumbile ya vipashio vinavyoifuata nomino. Hivyo, nomino katika Kisukuma inaweza kufuatwa na vivumishi, vioneshi, nambari, vivumishi vya idadi kwa jumla, virai vishirikishi na vishazi rejeshi vioneshi vikionesha miundo tofauti ya virai nomino. Kwa mfano, ameeleza kuwa vimilikishi na vioneshi vinaweza kukaa na vibainishi vingine vyote lakini vioneshi haviwezi kutokea mara tu baada ya nomino. Mifano ifuatayo hapa chini inadhihirisha ukweli huo: (Magashi, keshatajwa: 68-70)

Nomino	kimilikishi	Idadi	kioneshi	nambari	Kivumishi	Idadi
<i>Abhaana</i>	<i>Bhane</i>	<i>Bchoose</i>	<i>Abho</i>	<i>abhaatano</i>	<i>Abhawiza</i>	<i>abhakwandy</i> <i>a</i>
‘watoto’	‘wangu’	‘wote’	‘wale’	‘watano’	‘wazuri’	‘wa kwanza’

- 5) (a) Kirai kishirikishi kirejeshi
Abhashinyanga *abhagumanile*
‘Kutoka Shinyanga’ ‘wanaokuja’
‘Watoto wangu wote wale watano wazuri wa kwanza kutoka Shinyanga
wanaokuja’
- b) Nomino kimilikishi idadi nambari

<i>abhaana</i>	<i>bhane</i>	<i>abhataano</i>	<i>bhoose</i>
‘Watoto’	‘wangu’	‘wataano’	‘wote’

‘Watoto wangu watano wote’

c) Nomino	kimilikishi	idadi	nambari
<i>Abhaana</i>	<i>bhane</i>	<i>bhoose</i>	<i>abhataano</i>
‘Watoto’	‘wangu’	‘wote’	‘watano’

‘Watoto wangu wote watano’

Mifano hiyo katika (5a-c) imetuonesha miundo ya virai nomino katika Kisukuma inavyobeba vipashio hadi vinane na pia vioneshi visivyoweza kutokea mara tu baada ya nomino.

Naye Ndomba (2006) alichunguza muundo wa kirainomino katika Kisamatengo.

Alionesha kuwa katika Kisamatengo vibainishi vinavyofuata nomino hufikia vitano.

(Ndomba, keshatajwa: 76) kama ifuatavyo hapa chini:

0	1	2	3	4	5
Nomino	Kioneshi	Kimilikishi	Kivumishi	Kiunganishi na nomino	Kirejeshi
<i>Ma-si‘m aji’</i>	<i>Gala ‘haya’</i>	<i>Gangu ‘yangu’</i>	<i>Ma-keli ‘machafu</i>	<i>Gu-akiliba ‘kutoka katika kisima’</i>	<i>Ga-gapi ‘ a m b a y o yamechemshwa</i>

‘Maji yangu haya machafu kutoka katika kisima ambayo yamchemshwa’

Mfano wa hapo juu umeonesha jinsi nomino katika Kisamatengo inavyofuata na vibainishi vinavyofika vitano.

Pia Ndomba ameeleza kuwa vimilikishi na vioneshi vinaweza kubadilisha nafasi ikiwa viunganishi na vimilikishi vitafuata vioneshi na vimilikishi moja kwa moja. Lakini vivumishi na viunganishi haviwezi kufuata nomino kuu moja kwa moja. Hebu tuangalie mifano ifuatayo hapa chini, (Ndomba, keshatajwa: 77);

7) (a)

Nomino	Kimilikishi	Kioneshi	Ki u n g a n i s h i nomino	K i v u m i s h i kiunganishi
<i>mwa-na</i>	<i>Jw-aki</i>	<i>Jo-nzo</i>	<i>Jw-a kutembu</i>	<i>m-neni</i>
‘mtoto’	‘wake’	‘huyu’	‘anatoka Litembu’	‘mnene’

‘Mtoto wake huyu anatoka Litembu mnene’

(b)

Nomino	Kimilikishi	Kioneshi	kivumishi	Kiunganishi na nomino
<i>Mwa-na</i>	<i>Jw-aki</i>	<i>Jo-nzo</i>	<i>m-neni</i>	<i>Jw-a kutembu</i>
‘mtoto’	‘wake’	‘huyu’	‘mnene’	‘ a n a t o k a Litembu

‘Mtoto wake huyu mnene anatoka Litembu.’

Katika mifano hiyo hapo juu (7 a-b) mtafiti amedhihirisha jinsi vivumishi na viunganishi katika Kisamatengo vinavyobadilishana nafasi na jinsi ambavyo haviwezi kukaa mara tu baada ya nomino.

Utafiti mwengine wa virai nomino ni ule uliofanywa na Neekamiah (2010) aliandika juu ya muundo wa virai nomino katika lugha ya Kihangaza. Katika kazi yake ametuonesha miundo mbalimbali ya virai nomino inayojitokeza katika lugha hii.

Ametueleza kuwa katika Kihangaza, kirai nomino kinaweza kujitokeza katika miundo kumi tofauti. Akiitaja miundo hiyo miongoni mwake ni kama hii ifuatayo hapa chini; (Neekamiah: keshatajwa: 76-77)

- a) Nomino pekee: *umunhu 'mtu'*
- b) Nomino na Kivumishi: *umunhu mwiiza 'mtu mzuri'*
- c) Kioneshi na Nomino: *uriya munhu* ‘yule mtu’
- d) Nomino na kimilikishi na kivumishi: *umunhu wanje mwiiza 'mtu wangu mzuri'*

Mifano katika (8 a-d) imetuonesha baadhi ya miundo ya virai nomino inavyojitokeza katika lugha ya Kihangaza ikiwa na vibainishi vyake ambavyo kwa mujibu wa mtafiti vinaweza kubadilishana nafasi.

Aidha Neekamiah (keshatajwa) ametueleza kuwa virai nomino katika lugha ya Kihangaza vinaweza kuwa na mchomozo finyu pale nomino pekee inapokuwa kiini cha kirai nomino na wakati huohuo kinakuwa ni kirai. Tuangalie mifano ifuatayo kutoka Kihangaza katika (9) hapa chini:

- 9) a) *uumugore* yavyaay' umwaana ‘mwanamke amejifungua mtoto’
- b) *inka zirimwozirarya* ibyatsi ‘ng'ombe wanakula majani’

Mifano katika (9a-b) imetuonesha jinsi virai nomino vinavyoweza kuwa na mchomozo finyu. Nomino katika herufi mlazo zinasimama kama kiima cha kirai nomino pia zimesimama kama kirai kamili.

10) a) ißitaßo vyaaanje vyaraßuze ‘vitabu vyangu vimepotea’

b) ßiriiya ßitabo ßyaanje ßißiri ßimutuku ßyaraßuse

‘Vitabu vyangu viwili vyengine vyote vimepotea’

Mifano katika (10 a-b) katika herufi mlazo huonesha kirai nomino kuwa na mchomozo mpana wa nomino kuandamana na vibainishi zaidi ambavyo vimo katika kirai nomino. Mtafiti katika utafiti huu amebainisha iwapo hali kama hii inajitokeza pia katika virai nomino nya Kimakunduchi.

Rugemalira (2005) katika uchanganuzi wake wa sarufi ya Runyambo ambayo ni lugha ya Kibantu inayozungumzwa kaskazini magharibi mwa Tanzania. Katika uchanganuzi huo amedai kuwa nomino inawezekana kubainishwa kwa vibainishi vinne hadi sita ingawa vibainishi vinne vinaonekana vyenye kujitokeza mara kwa mara. Vibainishi hivi ni vimilikishi, nambari, vivumishi, na kadhalika. Vimilikishi kila mara vinatokea mara tu baada ya nomino na kishazi kirejeshi kinatokea mwisho wa mipangilio yote inayowezekana, nambari zinafuata vivumishi. Tuangalie mifano hapa chini;

2 a) *omontu + waaya + Oriya +atagamba*

‘Yule mtu wako asiyesema’

2b) *abhantu + banje +babiri +bahango*

‘Watu wangu wawili wakubwa’

Katika mifano ya hapo juu imetuonesha kuwa nomino inawezekana kubainishwa kwa vibainishi sita katika lugha mbali mbali za Kibantu. Kwa hiyo mtafiti katika utafiti huu ametaka kubainisha iwapo hali kama hii imejitokeza katika kirai nomino cha Kimakunduchi.

Pia ameeleza kuwa sentensi iliyobebwa na kirai nomino inatokea tu katika nafasi ya mwisho ya mipangilio yote inayowezekana wakati ambapo vipashio vingine kama vivumishi, nambari, virai vishirikishi na idadi jumuishi vinachukuliwa kwamba vinaweza kutokea katika nafasi yoyote kama inavyooneshwa hapa chini;

- 1) a) Kitabu changu kile.
- b) Kitabu kipyä kizuri
- c) Vitabu vingi vizuri.
- d) Watu wa Tanzania wanaokaa Ulaya.
- e) Watu wote wa Tanzania.

Mifano ya hapo juu imetuonesha mipangilio ya vipashio ndani ya virai nomino inavyojitokeza katika lugha mbali mbali za Kibantu. Katika utafiti huu nia yetu ilikuwa ni kuona kama lahaja ya Kimakunduchi ambayo ni lahaja ya Kiswahili kuna mfuatano unaofanana na huu au kuna mabadiliko yoyote.

Vilevile kwa upande wa muundo wa kirai nomino cha Kiingereza ameeleza kuwa unaonyesha tofauti kubwa ukilinganishwa na ule wa lugha za Kibantu. Kwa mfano; KN (B) (KV) N (KH) (KS) hapa KN ina muundo wa kutanguliza kibainishi na

/au kirai kivumishi ambapo lugha nyingi za Kibantu hutanguliza neno kuu (Rugemalira, 2007) kama katika jaduweli lililoelezwa na Lusekelo (2009) linalofuata hapo chini. Hata hivyo, muundo huu wa kirai nomino cha Kiingereza ulitusaidia kujuu kuwa kirai nomino kina mpangilio fulani katika lugha mbali mbali, hivyo kutupa changamoto za kuutafuta mpangilio wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi.

Lusekelo (2009) ameелееза mpangilio wa viandami vyat kirai nomino katika lugha mbali mbali za Kibantu kama unavyoonekana katika jaduweli hapo chini;

Jedwali Na. 2. 1 Mpangilio wa Viandami katika baadhi ya Lugha za Kibantu.

Lugha ya Kibantu	M pangilio wa Viandami	Mwandishi
Kikagulu	N + B + KV/KH	Petzell (2008)
Kimatengo	N + B + Ve + S	Ndomba(2006)
Mbugwe	(B) + N + (B) + Ve	Mous (2004)
Kingoni	N + B + V + KIA + B	Ngonyani (2003)
Kinyambo	N + B += Ve +S	Rugemalira (2005)
Kinyakyusa	N + (B) + (NUM/KIA) + (S)	Lusekelo (2009)
Kiswahili	N + B + V + B + NUM	Krifka (2005)
Kiswahili	(B) + N + B + (B) + (NUM) + V + (NUM)	Polome (1967)
Kibasaa	(B) + N + (B) + Ve + (B)	Hyman (2003)
Kimakuwa	(B) + N + (B) + (B) + Ve	Kisseberth (2003)
Kinen	N + V + KH	Mous (2003)
Kihehero	N + B + Ve	Elderkin (2003)
Kibantu	N + V + NUM + Ve	Nurse na Philppson (2003)

Chanzo: Lusekelo, (2009)

Kutokana na jedwali hilo tunaweza kubainisha kwamba kuna mipangilio mbalimbali ya viandami vya kirai nomino katika lugha za kibantu. Baadhi ya wanaisimu wanaona kwamba hakuna taratibu maalumu za mpangilio wa viandami vya kirai nomino katika lugha za Kibantu. Katika lugha hizi tunaona kuwa Kimbugwe, Kiswahili, Kibasaa na Kimakuwa huweza kutanguliza viandami kama vile vibainishi kabla ya neno kuu ambapo lugha zilizobaki hutanguliza neno kuu. Kiswahili kinaonekana kujitokeza pande zote mbili kikitanguliza vibainishi ama neno kuu. Kibainishi kimilikishi au kionyeshi huliandama neno kuu kwa lugha karibu zote hapo juu ukiondoa lugha ya Kinen ambayo neno kuu hufuatwa na kivumishi. Vilevile karibu lugha zote, kirai kihuishi na hasa kishazi rejeshi hujitokeza mwishoni. Mtafiti katika utafiti huu anataka kubainisha iwapo hali kama hii inajitokeza pia katika virai nomino vya Kimakunduchi.

Kijakazi (2012) katika uchanganuzi wake wa lahaja ya Kitumbatu ambayo ni mojawapo ya lahaja ya Kiswahili ambayo inazungumzwa katika kisiwa cha Tumbatu. Katika uchanganuzi wake amedai kuwa muundo wa msingi wa virai nomino ni nomino pekee au nomino ikifuatiwa na vibainishi vingine.

Pia (Kijakazi, keshatajwa) ameeleza kuwa katika muundo wa kirai nomino cha Kitumbatu, vivumishi vyote vinaweza kujitokeza mara tu baada ya nomino. Vivumishi hivyo vinaweza kuwa vya “sifa,” “idadi” au “rangi”. Mpangilio wa utokeaji wake ni kama unavyoonekana katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 2.2 Nafasi ya kivumishi

Nomino	Kivumishi	Kivumishi	Kivumishi
muhuzi (<i>muhuzi</i>)	mkongwe (<i>mzee</i>)	-	-
muyu (<i>mbuyu</i>)	mmoji (<i>mmoja</i>)	mnene (<i>mnene</i>)	-
nyumba (<i>nyumba</i>)	kul*u (<i>kubwa</i>)	zuri ‘zuri’	ngepe (<i>nyeupe</i>)
Kongwa (<i>tumbawe</i>)	girufi (<i>jeusi</i>)		

Chanzo: Uwandani

Katika jedwali hapo juu tunaona kuwa vivumishi vinatokea baada ya nomino na vinavyoweza kubadilishana nafasi.

Pia (Kijakazi, keshatajwa) ameeleza kuwa viwakilishi vinaweza kujitokeza kabla au baada ya nomino, lakini muundo wa msingi ni ule wa baada ya nomino katika virai nomino vya Kitumbatu na ule wa kabla ya nomino ni wa hiyari. Viwakilishi hivyo ni vya aina zinazobainishwa kimaana kama ‘vioneshi’ na ‘vimilikishi’. Kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini;

Jedwali Na. 2.3 Nafasi ya Vioneshi na Vimilikishi

vimilikishi	vioneshi	nomino	vimilikishi	Vioneshi
yakwe (<i>yake</i>)	-	shamba ‘shamba’	-	-
-	-	shamba ‘shamba’	yakwe (<i>yake</i>)	
-	kino (<i>hiki/huu</i>)	kiwamba ‘ukuta’ senti ‘sinia’	- -	- zilya (<i>zile</i>)
-	-	shana	lyangu (<i>langu</i>)	lilya (<i>lile</i>)

	‘shanuo’	
--	----------	--

Chanzo: Uwandani

Jedwali linaonesha viwakilishi vinavyobainishwa kama ‘vioneshi’ na ‘vimilikishi’ vikiwa na hiyari kutokea kabla au baadaya nomino katika muundo wa virai nomino vyta Kitumbatu. Pia viwakilishi hivyo vinaweza kufatana baada ya nomino.

Vilevile ameeleza kuwa kumejitokeza mfuatano mwingine wa kibainishi ‘kila’ ambacho kinatokea kabla ya N tu katika Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu.

Neekemiah (keshatajwa: 86)

Jedwali Na. 2.4 Nafasi ya Kibainishi ‘kila’ katika Lugha Tofauti.

	01	0	
	kila	nomino	tafsiri
Kihangaza	buru	munhu	kila mtu
Kimashami	wo	nndu	kila mtu
Kiswahili	kila	mtu	kila mtu
Kinyambo	buru	muntu	kila mtu

Chanzo: Neekamiah, (2010)

Jedwali hapo juu linaonesha utokeaji wa kibainishi ‘kila’ kabla ya nomino. Aidha Kijakazi (keshatajwa) ametueleza kuwa virai nomino katika lahaja ya Kitumbatu vinaweza kuwa na mchomozo finyu pale ambapo neno kuu kusimama peke yake na wakati huohuo kama kiini na kirai kamili cha kategoria husika. Tuangalie mifano ifuatayo kutoka katika lahaja ya Kitumbatu hapa chini:

- a) Mtima utuzu (*moyo umetulia*).
- b) Msembwe ukesha (*msewe ulipigwa usiku kucha*).
- c) Nahodha keshatekwa (*nahodha ameshapandisha tanga*).

Nomino zilizopigwa mstari hapo juu zimesimama kama ni maneno makuu ambayo ni viini na pia virai nomino ambavyo vinaonesha mchomozo finyu katika virai nomino vyta Kitumbatu.

Vilevile tumeelezwa kuwa kirai nomino katika lahaja ya Kitumbatu kinaweza kuwa na mchomozo mpana inahusu kirai kinachobeba neno kuu na kutanuliwa kwa kuongezewa vibainishi vingine zaidi. Tuangalie mifano ifuatayo hapa chini:

- a) wanafunzi waili waojakwenda mjini wamarudi (*wanafunzi wawili waliokwenda mjini wamerudi*).
- b) Nyumba ngepe zuri ya kulya Mkokotoni il*ungul*u (*nyumba nyeupe nzuri ya kule Mkokotoni imeungua moto*).

Mifano ya hapo juu inaonesha kirai nomino kinachobeba nomino (katika herufi mkozo) na vibainishi vingine katika muundo wake.

Mifano ya hapo juu inatuonesha mipangilio ya vipashio ndani ya virai nomino inavyojitokeza katika lugha mbali mbali za Kibantu. Katika utafiti huu nia ya mtafiti ilikuwa ni kuona kama lahaja ya Kimakunduchi ambayo ni lahaja ya Kiswahili kuna mfuatano unaofanana na huu au kuna mabadiliko yoyote.

Rijkhoff (2002) katika utafiti wake amechunguza virai nomino kwa kutumia vielelezo vya lugha 6000 au zaidi na kupendekeza kigezo cha kisemantiki ili kueleza miundo yao katika lugha yoyote ya asili. Inachunguza tabia za kisemantiki na mofosintaksia za vijenzi vya virai nomino. Amechambua kirai nomino kama ni muundo wa kitabaka ambao umekusanya vivumishi vinavyohusiana na sifa, idadi, pahala na “discourse.” Virai nomino na sentensi vinaweza kuwa na uchambuzi uliosawia, amedai kuwa, kwa sababu zote zina miundo sawa ya kisemantiki pamoja na mgawanyo sawa wa aina za vivumishi. Ameelezea kuwa dhana ya Seinsart au ‘mode of being’ kama ni mfano wa kirai nomino wa Aktionsart au ‘mode of action’ katika maana za kitenzi. Kazi ya Rijkhoff (2002) imemsaidia mtatifi kubainisha vipengele vya muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi.

Wabwire (2013) amechunguza virai nomino katika lugha ya Olukhayo na kubainisha muundo wa kirai nomino, dhima za kisintakisia za kirai nomino na kukieleza kirai nomino kwa kutumia nadharia ya Eksibaa. Virai nomino vilitambuliwa kutokana na sentensi kwa kutumia njia ya maelezo. Kazi ya Wabwire (2013) imemsaidia mtatifi kubainisha dhima za kisarufi za kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi.

Issah (2013) amechunguza muundo wa kirai nomino sahili katika lugha ya Dagbani na kueleza kuwa umeundwa na nomino ambayo neno kuu ni lazima, na aina nyengine za maneno ambazo si za lazima katika kirai nomino. Maneno haya ambayo si ya lazima kwa ujumla huifuata nomino kuu ya kirai nomino sahili na kwa hivyo huoneshwa kama kivumishi tamati (*post head modifier*). Vivumishi (*modifiers*),

vitarakimu (*numerals*), vioneshi (*demonstratives*), vibainishi (*determiners*) na viujazo (*quintifiers*) huchambuliwa kama vivumishi nomino vyatia kirai nomino sahili katika lugha ya Dagbani. Vivumishi hutoa habari fulani za kisarufi na za kisemantiki kuhusu nomino ambayo imefanyiwa marekebisho. Japo kuwa kirai nomino katika Dagbani huweza kuchukua vivumishi nomino tamati vingi, vivumishi hivi vimepangwa kwa sababu kila kivumishi kinayo nafasi yake kisintaksia.

Inusah (2015) katika utafiti wake amechunguza muundo wa kirai nomino katika lugha ya Safaliba ambayo ni lugha ya jamii ya Kigur inayozungumzwa kaskazini mwa Ghana. Katika uchunguzi huo mtafiti alibaini kuwa kirai nomino katika lugha ya Safaliba kimeundwa na nomino kama neno lake kuu na maneno ya ziada mengine ni kivumishi awali (pre modifier) na kivumishi tamati (post modifier). Vivumishi na vibainishi vinachambuliwa kama vivumishi vyatia kirai nomino katika lugha ya Safaliba huchukua vivumishi tamati vingi ambavyo vimepangiliwa katika mpango maalumu kwa sababu kila kivumishi kina nafasi yake maalumu ya kisintaksia. Kazi ya Issah (2013) na Inusah (2015) imemsaidia mtafiti kubainisha vipengele vyatia muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi.

Uchambuzi uliofanywa hapo juu wa kazi tangulizi unaonesha kuwa watafiti wote walijikita zaidi katika kuangalia vipashio vyatia kimuundo vyatia kirai nomino katika lugha husika, lakini hawakuangalia dhima za kisarufi za kirai nomino. Upungifu huo ndio uliofanya kuwepo na pengo la utafiti ambalo utafiti huu umelishughulikia.

Kwa ujumla tunaona kuwa muundo wa virai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi bado haujafanyiwa kazi vya kutosha. Hivyo basi kuna haja ya kuanza kuangalia miundo ya virai nomino katika lahaja hii ili kuweza kuona inajibainishaje. Kazi hii imefanywa kwa kina katika sura ya nne. Pia tunaona kuwa kuna mabadiliko na vipingamizi vya utokeaji wa vipashio ndani ya virai nomino katika lugha mbalimbali za Kibantu. Hoja hii inaonesha kuwapo haja ya kufanya utafiti katika kipengele hiki kwani kunaweza kuonekana hali tofauti za virai nomino katika lahaja za Kiswahili na ile tulioizoea katika Kiswahili Sanifu kama baadhi ya tofauti zinavyoonekana katika vipengele vingine vya kiisimu kama vile, vipengele vya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia.

2.4 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya sarufi miundo virai na dhana yake maarufu ya mahusiano ndani ya kirai inayojulikana kama ***nadharia ya eksibaa***. Kwa mujibu wa TUKI (1990), sarufi miundo virai ni kitengo cha sarufi geuza maumbo zalishi, ambacho hujikita katika matumizi ya sheria chache kuzalisha sentensi nyingi zisizo na kikomo, ambazo zina usarufi na hata zile ambazo hazijawahi kutungwa. Sheria zinazotumiwa katika sarufi miundo virai si elekezi kama zile za sarufi mapokeo bali huonyesha na kufafanua viambajengo vya sentensi. Sheria hizi husaidia katika kudokeza maana ya sentensi. Sheria miundo virai hujikita katika uandikaji upya wa sheria za sarufi ambazo hudhihirisha nafasi na uamilifu wa viambajengo vya sentensi, kuanzia kiambajengo kikubwa (sentensi) hadi kiambajengo kidogo (mofu). Mwanzilishi wa nadharia ya sarufi miundo virai ni Noam Chomsky.

2.4.1 Nadharia ya Eksibaa

Eksibaa ni nadharia ya sarufi miundo virai iliyoendelezwa badala ya ile ya sarufi miundo. Hoja muhimu katika nadharia hii ni kwamba sheria za sarufi miundo virai hazina budi kudhibitiwa na kwamba kategoria zaidi za virai hazina budi kuongezwa. Kwa mfano, katika kategoria ya virai nomino kuna haja ya kuingiza kategoria nyengine ambazo ni kubwa kuliko nomino lakini ni ndogo kuliko kirai (Massamba 2004). Kwa mujibu wa Leffel na Bouchard (1991), Eksibaa husimama kama neno kuu ambalo linaweza kuwa nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi na kadhalika katika muundo wa kirai, nayo husimama kama muundo kiini. Hivyo kirai cha kategoria fulani kitakuwa na neno ambalo ndicho kiini cha kirai hicho. Kwa mfano, kirai nomino (KN) kiini chake kitakuwa ni nomino (N) ambayo itachukuwa nafasi ya X katika muundo wa kirai itakavyotumika katika utafiti huu. Vilevile kistari juu ya eksibaa humaanisha vijalizo ambavyo hulifuata neno kuu katika muundo wa kirai. Vistari hivyo vitawenza kuwa vivumishi, vielezi, sentensi na kadhalika. Kiini cha kirai ndicho kinachopanga muundo wa kirai chochote kiwacho.

Kwa kutumia nadharia hii tumeweza kuona muundo wa kirai ukiwa na mchomozo finyu. Hali hii hujitokeza pale neno kuu linaposimama peke yake kama kirai na pia kama kiini cha kirai hicho katika muundo kama huo tulioueleza. X huwa na kipeo sifuri na kwa upande wa kirai nomino N huwa na sifuri vilevile. Tuangalie mifano ifuatayo hapa chini kutoka Kiswahili.

- a) Mtoto anacheza.

b) Mwalimu anafundisha.

Katika mifano hii, maneno yaliyopigiwa mstari ni nomino ambazo zimesimama kama neno kuu la kirai nomino na wakati huohuo limesimama kama kirai nomino katika fungu hizo.

Pia eksibaa inaeleza kuwa muundo wa kirai unaweza kuwa na mchomozo mpana wa kibainishi kimoja au zaidi. Hali hii hujitokeza kwa neno kuu kama nomino kufuatwa na kibainishi kingine katika muundo wa kirai. Mifano ifuatayo kutoka lugha ya Kiswahili inafafanua dhana hii:

- a) Kuku aliyetwa jana amekufa.
- b) Ng'ombe wa maziwa na kuku wa nyama watapewa chanjo.

Tungo zilizopigiwa mistari zinatuonesha kirai nomino kinavyoweza kuwa na mchomozo mpana kwa kuchukua vibainishi zaidi.

Kwa kuangalia umuhimu wa kuchambua sentensi na virai kwa kutumia nadharia inayoangalia kategoria kama hii ya Eksibaa, sarufi muundo virai imeweza kubainisha vipashio vinavyounda virai nomino vya Kimakunduchi. Kwa sababu katika nadharia hii tunaelezwa kuwa sentensi imeundwa kwa mpangilio maalumu ambao huwa na virai ambavyo vimewekwa katika seti maalumu ya kategoria ambapo kategoria ya virai ni sehemu muhimu. Neekemiah (2010:18), akimnukuu Radford (1981) anaeleza kuwa;

Ni vizuri tukachanganua miundo ya kisintaksia kwa kuegemeza uchanganuzi wetu kwenye mkabala wa kategoria kirai na si kwenye mkabala wa maneno.

Kutokana na hali hiyo, mtafiti katika utafiti huu ametumia nadharia hii kujaribu kuonesha miundo mbalimbali ya virai nomino vya Kimakunduchi. Halikadhalika, nadharia imetuwezesha kuona vibainishi vya nomino vikifuata nomino. Pia imetuwezesha kuona na kubainishi vibainishi vinavyoweza kutokea kabla na baada ya nomino. Vilevile imemsaidia kuona mpangilio wa vibainishi hivyo katika muundo wa virai nomino na hali ya kukubalika kwa utokeaji wa vibainishi kulingana na miundo mbalimbali ya virai nomino inayojitokeza katika Kimakunduchi.

Aidha, nadharia hii ina njia mbili kuu za kuchanganua miundo ya kisintaksia ambayo ni matawi na mabano. Katika utafiti huu miundo ya virai nomino imechanganuliwa kwa kutumia matawi ya kisintaksia kwa sababu, matawi haya huonesha uhusiano wa moja kwa moja wa vipashio vinavyounda virai.

Kwa kawaida matawi haya huchomoza kutoka kwenye viambajengo. Kila kifundo huwakilisha kiambajengo kilichomo katika muundo wa kirai au sentensi. Kifundo kinachokaa juu katika mti wa kisintaksia hujulikana kama kifundo cha juu na ndicho kiambajengo kikubwa. Kifundo hiki ndicho hutawalia vifundo vya chini ambavyo hubeba viambajengo vidogo. Katika matawi haya vifundo vya chini hupangana kisafu kuonesha kipashio kipi hutangulia kingine.

Vifundo viliwyopangana kisafu hujulikana kama vifundo dada ambavyo hutawaliwa moja kwa moja na kifundo cha juu (Fromkin, 2000). Kwa mfano, ikiwa KN kitakuwa ni kifundo cha juu na kitatawalia N na V ambavyo vitakuwa ni vifundo nya chini na pia ni viambajengo vidogo. Taratibu hizi za mpangilio wa vifundo nya viambajengo kiwima na kisafu zimeibua dhana mbili muhimu zinazojulikana kama “utawalia” na “utangulizani”. Utawalia huhusu uhusiano wa kifundo cha juu na cha chini yake. Uhusiano huo unaoneshwa kwa mistari, huonesha kuwa kifundo cha chini ni kiambajengo cha kifundo cha juu. Kifundo cha juu huweza kutawalia kifundo cha chini kimoja, viwili, vitatu au zaidi.

Utangulizani kwa upande mwingine huonesha uhusiano wa vifundo kisafu. Hapa vifundo nya chini vinavyotawaliwa moja kwa moja na kifundo cha juu huitwa dada. Vifundo dada hujipanga katika daraja sawa kisafu na huwa jirani pale vinapohusika vifundo viwili vinavyotawaliwa moja kwa moja na vifundo nya juu (Fromkin 2000). Hebu tuangalie uchanganuzi wa muundo wa kirai nomino katika Kiswahili Sanifu kwa njia ya matawi ya kisintaksia hapo chini ili tuweze kuona hali tuliyioieleza, mfano; Mtoto mzuri

KN

N

V

Mtoto	mzuri
-------	-------

Njia nyingine inayotumika katika kuchanganua muundo wa kirai ni ile ya mabano. Njia hii huhusu matumizi ya mabano mraba ambayo hutenganisha vipashio vyote vilivyomo katika kiambajengo kwa kutumia mabano hayo. Kiambajengo huvidhibiti viambajengo vidogo vinavyounda kirai au sentensi. Hebu tuangalie mfano ufuatao ili tuone uchanganuzi wa muundo wa kirai nomino kwa njia ya mabano kutoka Kiswahili sanifu hapa chini:

Mwanafunzi hodari

[KN [N *mwanafunzi*] [V *hodari*]].

Tukilinganisha njia hizo mbili za kuchanganua muundo wa kirai nomino tunaona kuwa njia ya matawi ya kisintaksia ni nzuri katika kuchanganua miundo ya viambajengo vya kirai nomino katika Kimakunduchi kwa vifundo kutawaliana na kutangulizana.

Njia hii inaonekana kuwa ni nzuri zaidi kwani imetumiwa na Massamba na wenzake (2009) kuchanganua miundo ya virai katika Kiswahili sanifu. Hivyo, nadharia ya sarufi muundo virai kwa kutumia kifaa tumizi cha Eksibaa bila shaka imewezesha kuchanganua na kubainisha kwa uwazi vipengele vya muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi.

2.5 Hitimisho

Sura hii imejadili mapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha nadharia. Mwanzo kabisa imeelezea mapitio kuhusu nadharia ya kirai nomino, tafiti tangulizi zilizofanywa na wataalamu kuhusu kirai nomino ili kutafuta pengo ambalo halikushughulikiwa kwa kina na wataalamu hao. Pia imeainisha nadharia ya sarufi miundo virai iliyoasisiwa na Noam Chomsky ambayo ni nadharia ya Eksibaa iliyoongoza utafiti huu ili kuweza kubainisha kiini cha kirai nomino cha Kimakunduchi.

SURA YA TATU**MBINU ZA UTAFITI****3.1 Utangulizi**

Sura hii inajadili mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu ambapo inaeleza mahala pa utafiti, watoa taarifa, sampuli iliyotumika, mbinu za ukusanyaji data, uchanganuzi wa data, vifaa au zana zilizotumika katika utafiti huu.

3.2 Mkabala wa Utafiti

Utafiti huu umefuata muundo wa kimaelezo katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Mtindo huu ni muafaka katika utafiti huu kwa sababu lengo la utafiti huu ni kubainisha muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi, ambao umejibainisha vizuri zaidi ulipoelezwa kwa kutumia maeleo kulingana na data zilizopatikana kutoka kwa watafitiwa ili kuweza kulifiki lengo hilo.

3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika Makunduchi katika mkoa wa kusini Unguja ambako ni eneo la asili la wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi. Kutohana na eneo hili kuwa na shehia nyingi, mtafiti amechagua shehia tatu nazo ni shehia ya Kiongoni, shehia ya Nganani na shehia ya Mzuri. Kwa vile lahaja hii haina maandiko mengi na inatumika zaidi kwa mazungumzo kwa hiyo mtafiti ameona ni vyema kutumia mazungumzo ya ana kwa ana na wanakijiji kwa ajili ya kupata data. Mtafiti amefanya utafiti katika shehia hizi kwa sababu amepata data kutoka kwa wazawa

ambao wana uweledi wa lajaja hii na kuweza kupata ufanuzi wa kina juu ya muundo wa kirai nomino katika lajaja ya Kimakunduchi.

3.4 Kundi Lengwa

Kwa mujibu wa Walliman (2011) kundi lengwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika kufanyiwa utafiti (vinavyotafitiwa) yaani watu, taasisi, vitu au matukio. Katika utafiti huu kundi lengwa ni wakaazi wote wa Makunduchi ambao ni watumiaji wa asili wa lajaja hii. Wakaazi hawa wanapatikana katika shehia tatu ambazo ni shehia ya Kiongoni, shehia ya Nganani na shehia ya Mzuri. Walengwa hao walikuwa ni watu wazima wenye umri wa kati na vijana wanawake na wanaume. Tumechagua walengwa kwa vigezo maalumu vikiwemo uweledi wa lugha mbili, umri wa ukaazi au uzawa (lugha mama) na wataalamu wa isimu kama wanafunzi waliomaliza vyuoni pamoja na wakufunzi ambao ni wazawa kutoka katika shehia hizo. Hivyo katika jumla ya walengwa wote ni walengwa sitini (60) tu waliteuliwa kama sampuli ya utafiti, thelathini walikuwa ni wanawake na thelathini ni wanaume kama inavyooneshwa katika mada ndogo ifuatayo. Data zilizotolewa na walengwa hao ndizo zilizotumika katika utafiti huu.

3.5 Sampuli na Usampulishaji

3.5.1 Sampuli.

Sampuli ni idadi au sehemu ndogo inayotokana na kundi kubwa la watoataarifa wanaochaguliwa kuwa wawakilishi wa kundi kubwa (Prewitt,1980). Utafiti huu umehusisha sampuli ya watu sitini (60), thelathini walikuwa ni wanawake na thelathini ni wanaume, watu ishirini (20) kutoka kila shehia.

3.5.2 Mchakato wa Usampulishaji.

Kwa mujibu wa Sigh (2007), usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Sampuli huchaguliwa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na nasibu (usampulishaji nasibu) na isiyo nasibu.

Utafiti huu umetumia sampuli kusudio hii ni aina ya usampulishaji ambayo mtafiti amechagua sampuli kulingana na malengo maalumu (Mlyuka, 2011). Kama ilivyoelezwa na Kothari (2009) kuwa uzuri wa utafiti ni kwa mtafiti kuchagua watoa taarifa wanaofaa kwa utafiti wake. Hivyo, sampuli kusudio imemsaidia mtafiti kupata watoa taarifa anaowataka. Utafiti huu umehusisha watoa taarifa sitini (60), thelathini ni wanawake na thelathini ni wanaume, wazee na vijana wenye umri wa kati ya miaka 30 na 70. Uteuzi wa watafitiwa wa umri huu ulifanywa kwa kuzingatia kuwa wazungumzaji wa umri huu wana ujuzi mkubwa wa lahaja hii; kwa hiyo taarifa watakazotoa zitakuwa za ukweli na za kuaminika. Uteuzi huu wa sampuli umezingatia muundo wa mada ulivyo, ambao umeonekana kuhitaji uelewa japo mdogo wa isimu ya lugha. Kama tunavyojua kwamba umuhimu wa sampuli unategemea tabia mbalimbali za mada inayoshughulikiwa. Ikiwa mada ina mawanda makubwa au ina tabia mbalimbali basi sampuli huwa ni kubwa, lakini kama mada imejikita katika tabia moja sampuli inayochaguliwa inatakiwa iwe na ufanisi (Prewitt, 1980). Kutokana na hali hiyo muundo wa virai nomino katika lugha

umeonekana kuwa ni wa tabia funge kuliko mada inayohusu tabia za watu. Hivyo basi, mtafiti ameridhika kuwa sampuli ya watu sitini itakuwa na ufanisi.

3.6. Mbinu za Ukusanyaji Data

Mbinu za ukusanyaji data ni mbinu ambazo mtafiti huzitumia ili kupata data za utafiti. Kitchin na Tale (2000) wanaeleza kuwa kuchagua mbinu ya kukusanya data si kuchagua mbinu yoyote inayoonekana rahisi kuitumia bali ni kuchagua mbinu inayojitosheleza na inayohusiana na kile unachokitafiti. Kwa kuwa lahaja hii haina maandiko kwa hiyo mtafiti aliona mbinu muafaka ya kukusanya data ni hojaji na uchunguzi makini kwa kupitia shughuli za kijamii kwa mfano mwaka kogwa, harusi, maziko na kadhalika kwa ajili ya kupata uthabitit wa data zilizohitajika katika utafiti huu.

3.6. 1 Uchunguzi makini

Kwa mujibu wa Kothari (2004) uchunguzi makini ni mbinu anayotumia mtafiti katika kuangalia moja kwa moja tukio, jambo au hali katika jamii. Njia hii ni maalumu kwa kuchunguza maisha na tabia za watu katika jamii. Katika utafiti huu mtafiti alitumia uchunguzi makini kupata data kwa kushiriki katika shughuli mbalimbali za jamii (ikiwemo sherehe za mwaka kogwa, sherehe za harusi, maziko na kadhalika).

Uteuzi wa njia ya uchunguzi makini katika utafiti huu ulifanywa kwa sababu zifuatazo; kwanza ilimuwezesha mtafiti kupata taarifa mbali mbali ambazo

asingeweza kuzipata kwa kutumia njia nyingine. Pili, njia hii hupunguza uwezekano wa mtafiti kuingiza hisia binafsi.

3.6.2 Hojaji

Hojaji ni mbinu ya kukusanya data ambayo mtafiti huandika maswali na baadaye huwapa watoa taarifa ili wayajibu na kumrudishia (Kothari, keshatajwa). Kwa maelezo ya Walliman (2011) maswali ya hojaji yako ya aina mbili. Aina ya kwanza ni maswali fungo ambayo hutoa fursa kwa watafitiwa kuchagua jawabu. Aina hii ni rahisi kujibu na kuchanganua. Pia inasaidia kupata majibu mahususi na huepusha upendeleo. Aina ya pili ya maswali ya hojaji ni yasiyo fungo, ambayo hutoa fursa au uhuru kwa watafitiwa kueleza wanachokijua. Pia, husaidia kupata taarifa nyingi zaidi. Mbinu ya hojaji iliyotumika katika utafiti huu imejumuisha aina zote mbili za maswali, yaani maswali fungo na yasiyo fungo ili kuepusha mapungufu yaliyoweza kutokea katika mbinu hizi mbili, ikizingatiwa kila moja ina mapungufu yake. Hivyo, mbinu hizi mbili zikitumika kwa pamoja kila moja husaidia kuziba mapungufu ya nyenziwe. Mtafiti alienda na hojaji hizo kwa watoa taarifa na kuwataka wabertilishe sentensi kutoka Kiswahili sanifu na kuwa katika lahaja ya Kimakunduchi. Pia mtafiti amejaza hojaji hizo kwa wale wasiojua kusoma na kuandika na wanaojua na kuelewa wamejaza wenyewe.

Katika utafiti huu mbinu ya hojaji ilionekana kuwa inafaa kwa sababu zifuatazo; kwanza, inawezesha kukusanya data katika kundi kubwa la watu kwa muda mfupi sana. Pili, njia hii ni rahisi na ya haraka katika kukusanya na kuchanganua data.

3.7 Mkabala wa Kimaadili ya Utafiti

Mkabala wa kimaadili ya utafiti unahusu msingi wa kanuni za kimaadili kwa mada mbalimbali zinazohusiana na utafiti wa kisayansi. Hii pamoja na kubuni na utekelezaji wa utafiti unaoshirikisha majaribio ya binadamu ya nyanja mbalimbali za kashfa za kielimu, pamoja na makosa kadhaa ya kisayansi (kama udanganyifu, upotoshaji wa data na wizi), utangazaji, udhibiti wa utafiti, nk.

Mambo ambayo mtafiti aliyazingatia katika utafiti huu ni kupata kibali au ridhaa ya kufanya utafiti, kujadiliana na kundi lengwa juu ya utafiti wake ili kuepusha matatizo, kuwa wazi katika utafiti wake ili kupata taarifa kwa urahisi, kulinda haki za watu vilevile faragha na usikivu, kuheshimu usiri wa wale waliohusika katika uchunguzi pia kuweka siri zao na utambulisho wao, kuwa muaminifu na muadilifu katika kazi yake, kuelewa sheria za nchi kuhusiana na utafiti n.k. (Shaw et al.2009).

3.8 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data za utafiti huu ulifanywa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo, ambao ni stabilifu katika utafiti unaolenga kupata taarifa kutokana na maoni na hisia binafsi za walengwa wa utafiti. Mkabala huu wa uchanganuzi umependekezwa kwa sababu data zilizokusanywa zipo katika hali ya maelezo. Kombo na Tromp (2006) wanaeleza kuwa uchambuzi wa data kwa njia ya maelezo umetumika katika tafiti za kimaelezo kama vile tafiti za kutafuta mitazamo au uelewa na mawazo ya watu juu ya jambo fulani. Wanaendelea kueleza kuwa, kwa kawaida uchambuzi wa aina hii hautumii ukokotozi wa data kwa kiasi kikubwa. Mkabala huu wa uchanganuzi wa

data ya utafiti umechaguliwa kwa sababu lengo la utafiti huu lilikuwa kubainisha vipengele vyta muundo wa kirai nomino, kuchanganua utaratibu / mpangilio wa vipengele katika kirai nomino na kubainisha dhima za kisarufi za kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi, kutokana na mawazo, maoni, na maono ya wazungumzaji asilia.

3.9 Vifaa vyta Utafiti

Utafiti huu umetumia vifaa kama kalamu, karatasi, kinasa sauti ili kurekodi majibu ya watoataarifa, shajara na kompyuta.

3.10 Hitimisho

Sura ya tatu imefafanua namna utafiti ulivyofanyika; hususani imeelezea muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa pamoja na sampuli na usampulishaji. Vilevile katika kufikia malengo ya utafiti huu sura hii imeainisha mbinu ya ukusanyaji na uchambuzi wa data pia imeeleza mkabala wa kimaadili ya utafiti, vilevile data zilizokusanywa kupitia mbinu hizo zimechambuliwa kwa mkabala stahilifu ambao hutumia maelezo katika uchambuzi wa data.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kuchambua data zilizokusanywa juu ya muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi. Uchanganuzi unafanywa kwa kuzingatia malengo mahsusini ya utafiti; ambayo yalikuwa ni pamoja na kubainisha vipengele vya muundo wa virai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi; kuelezea utaratibu / mpangilio wa vipengele vya muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi; na kubainisha dhima za kisarufi za kirai nomino cha lahaja ya Kimakunduchi.

4.2 Muundo wa Virai Nomino katika Lahaja ya Kimakunduchi

Lengo la kwanza la utafiti lilikuwa kubainisha vipengele vya muundo wa virai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi. Utafiti huu umebaini kuwa katika lahaja ya Kimakunduchi viro virai nomino vya aina nane nazo ni; Nomino moja pekee, nomino na kivumishi, kiwakilishi na kivumishi, kiwakilishi pekee, nomino na kishazi tegemezi, kitenzi jina na kivumishi, kitenzi jina na nomino, kivumishi na kishazi tegemezi vumishi. Katika sehemu ifuatayo tunawasilisha data zinazoonesha miundo ya aina mbalimbali za virai nomino vilivyobainishwa vya lahaja ya Kimakunduchi.

4.2.1 Kirai Nomino cha Muundo wa Nomino moja Pekee (N)

Aina ya kwanza ya virai nomino vya Kimakunduchi ni kirai nomino cha nomino moja pekee. Aina hii ya kirai nomino huundwa na neno moja tu ambalo ni nomino, kama inavyodhihirishwa katika mifano ifuatayo;

Jedwali Na. 4.1 Kirai Nomino cha Muundo wa Nomino moja Pekee (N)

Kimakunduchi	Kiswahili sanifu
<i>Wavulyana</i> wauku	Wavulana wameondoka
<i>Chui</i> kanakulya	Chui anakula
<i>Bwe</i> ligu	jiwe limedondoka
<i>Vua / mboji</i> ishamiri	mvua imeshamiri
<i>Mram / shemeji</i> kaja	shemeji kaja
<i>Shanuo</i> lyaga	shanuo limepotea

Chanzo: Uwandani, (2016)

Katika sentensi za hapo juu virai nomino vya muundo wa neno moja ni *wavulyana, chui, bwe, vua (mboji), mram (shemeji) na shanuo* ambavyo vimesimama kama neno kuu la kirai nomino na vimejengeka kwa nomino moja tu.

Data hizi zinalingana na maelezo ya Kijakazi (2012) kuhusu muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kitumbatu ambao unaonesha kuwa kuna kirai nomino chenye neno kuu peke yake. Pia Neekamiah (2010) naye aliandika juu ya muundo wa kirai nomino katika Kihangaza naye alieleza kuwa muundo huo pia upo katika miundo ya virai nomino vya lugha hiyo. Vile vile Rugemalira (2005) katika uchanganuzi wake wa sarufi ya Kiyambo naye ametuonesha kuwa kuna muundo wa kirai nomino cha neno kuu peke yake. Uchanganuzi wa kirai nomino cha nomino moja pekee una muonekano ufaustao.

N'

Bwe

4.2.2 Kirai Nomino Cha Nomino na Kivumishi (N + V)

Aina ya pili ya virai nomino vya Kimakunduchi ni kirai nomino na kivumishi. Aina hii ya kirai nomino huundwa kutokana na nomino na kivumishi kimoja au zaidi, kama inavyooneshwa katika data zifuatazo ;

Jedwali Na. 4.2 Kirai Nomino Cha Nomino na Kivumishi (N + V)

Kimakunduchi	Kiswahili sanifu
<i>Wanakele wadogo wakorofî waga</i>	Watoto wadogo wakorofî wamepotea
<i>Kuku wengi weupe wanunuligwa</i>	Kuku wengi weupe wamenunuliwa
<i>Mwanakele mzuri kanaoga</i>	Mtoto mzuri anaogopa
<i>Nguo nydingi nyeupe mbovu zifuligwa</i>	Nguo nydingi nyeupe zimefuliwa
<i>Mjiti mkubwa ukatiki</i>	Mti mkubwa umekatika

Chanzo: Uwandani,(2016)

Katika mifano ya hapo juu muundo wa kirai nomino uliohusisha nomino na kivumishi kimoja ni *mwanakele mzuri, mjiti mkubwa* na mifano ya virai nomino vyenye nomino moja na vivumishi zaidi ya kimoja ni *wanakele wadogo wakorofî, kuku wengi weupe, na nguo nydingi nyeupe mbovu.*

Muundo wa kirai nomino unaoundwa kutokana na nomino na kivumishi unatumika katika lugha nyingi kwa mfano Mtallo (2015) ameonyesha muundo huo katika lugha ya Kiuru, mmoja ya mifano aliyoitoa kudhihirisha dhana hii ni; *Maembe ang'anyi*

mnu [maembe mengi sana]. Pia Neekamiah (2010) nae ametuonesha muundo huo katika lugha ya Kihangaza, mmoja ya mifano aliyoitoa kudhihirisha dhana hii ni; *Umunhu mwiiza* [mtu mzuri].

Uchananuzi wa kirai nomino cha nomino na kivumishi una muonekano ufaatao.

KN

N

N

V

Mwanakele mzuri

4.2.3 Kirai Nomino cha Kiwakilishi Pekee (W)

Aina hii ya kirai nomino huundwa kwa neno moja tu ambalo ni kiwakilishi, kama inavyodhihirishwa katika data zifuatazo;

Jedwali Na. 4.3 Kirai Nomino cha Kiwakilishi Pekee (W)

Kimakunduchi	Kiswahili sanifu
<i>Suwe nyi wanafunzi</i>	Sisi ni wanafunzi
<i>Mie nkazwa nyi kusoma hadithi</i>	Mimi ninapenda kusoma hadithi
<i>Weye hulikazwa nyi hisabu</i>	Wewe hupendi hisabu
<i>Nyuwe mchakuja kesho</i>	Nyinyi mtakuja kesho
<i>Yeye katende mtihani vizuri</i>	Yeye kafanya mtihani vizuri
<i>Wao wachakuja kesho</i>	Wao watakuja kesho

Chanzo: Uwandani, (2016)

Mifano ya hapo juu inaonesha virai nomino vya lahaja ya Kimakunduchi vyenye muundo unaohusisha kiwakilishi pekee navyo ni; *suwe, mie, weye, nyuwe, yeye* na *wao*.

Uchanganuzi wa kirai nomino cha nomino na kiwakilishi pekee una muonekano ufaauatao.

KN

W

kesho

4.2.4 Kirai Nomino cha Nomino na Kishazi Tegemezi (N + Kish - teg)

Aina nyingine ya virai nomino vya Kimakunduchi ni kirai cha nomino na kishazi tegemezi. Aina hii ya kirai nomino huundwa kutokana na nomino na kishazi tegemezi, kama inavyobainishwa katika data zifuatazo;

Jedwali Na. 4.4 Kirai Nomino cha Nomino na Kishazi Tegemezi (N + Kish - teg)

<i>Mbuzi mwachinjwa juzi</i> kevu kanavukutwa	Mbuzi aliyechinjwa juzi alikuwa anaumwa.
<i>Mwalimu ayeuka mwaka jana</i> kaja vingine	Mwalimu aliyeondoka mwaka jana amerudi tena
<i>Mwari mwakwiba nguo</i> kagwiwa	Msichana aliyeiba nguo amekamatwa
<i>Baba avyouka jana</i> kevu nlala	Baba alipoondoka jana nilikuwa nimelala
<i>Kamusi iyounuligwa jana</i> ibwa	Kamusi niliyonunuliwa jana imeibiwa

Chanzo : Uwandani, (2016)

Katika mifano ya hapo juu maneno yaliyoandikwa kwa herufi mlazo ni muundo wa kirai nomino uliohusisha kirai nomino na kishazi tegemezi nayo ni ; *Mbuzi mwachinjwa juzi, Mwalimu ayeuka mwaka jana, Mwari mwakwiba nguo, Baba avyouka jana na Kamusi iyonunuligwa jana.*

Matokeo haya yanalingana na yale ya utafiti wa Wozna na Wilson (2005) katika uchunguzi wao wa lugha ya Seimat kutoka Papua New Guinea. Wao walibainisha kuwa lugha ya Seimat ina virai nomino ambavyo vimeundwa kutokana na nomino na kishazi tegemezi kwa mfano ; Kalu huali seilon (ti) kalu ilowi [*tutawasaidia watu tulioaalika*], maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi hiyo ni kishazi tegemezi. Uchanganuzi wa kirai nomino cha nomino na kishazi tegemezi una muonekano ufauatao ;

KN

N'

N Kish - teg

Mwari mwakwiba nguo

4.2.5 Kirai Nomino chenye Muundo wa Kitenzi Jina (TJ)

Aina nyingine ya virai nomino katika Kimakunduchi ni ile ya nomino zenyenye muundo wa kitenzi jina. Aina hii ya kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi huundwa kutokana na kitenzi jina pekee, kitenzi jina ni kitenzi kinachofanya kazi kama jina, data za hapa chini zinaonyesha nomino zenyenye muundo wa kitenzi jina kama ilivyobainishwa katika tungo za Kimakunduchi:

Jedwali Na. 4.5 Kirai Nomino chenyenye Muundo wa Kitenzi Jina (TJ)

Kimakunduchi	Kiswahili sanifu
<i>Kwimba</i> kuwapendezesha wengi	Kuimba kunawapendezesha wengi
<i>Kwiba</i> kuwachukizi watu	Kuiba kunawachukiza watu
<i>Kucheza</i> kuwafurahisha sana	Kucheza kunawafurahisha sana
<i>Kuuka</i> kuchaleta balaa	Kuondoka kutaleta balaa
<i>Kucheka</i> kuchakera wengi	Kucheka kutakera wengi

Chanzo: Uwandani, (2016)

Katika mifano ya hapo juu maneno yaliyoandikwa kwa herufi mlazo ni muundo wa kirai nomino uliohusisha kitenzi jina pekee nao ni; *kuuka, kucheza, kwimba, kwiba na kucheka*.

Uchanganuzi wa kirai nomino cha kitenzi jina una muonekano ufaulatao;

KN

TJ

Kuuka

4.2.6 Kirai Nomino cha Muundo wa Kitenzi Jina na Kivumishi (TJ+ V)

Aina hii ya kirai nomino huundwa kutokana na kitenzi jina na kivumishi kama inavyobainishwa hapa chini;

Jedwali Na. 4.6 Kirai Nomino cha Muundo wa Kitenzi Jina na Kivumishi (TJ+ V)

Kimakunduchi	Kiswahili sanifu
<i>Kuuka kwake kuwafurahisha wengi</i>	Kuondoka kwake kunawafurahisha wengi
<i>Kucheza kwao kuchaleta balaa</i>	Kucheza kwao kutaleta balaa
<i>Kwimba kwake kuwapendezesha wengi</i>	Kuimba kwake kunawapendezesha wengi
<i>Kwiba kwao kuwachukiza wengi</i>	Kuiba kwao kunawachukiza wengi
<i>Kucheka kwake kuwachechesha wote</i>	Kucheka kwake kunawachechesha wengi

Chanzo : Uwandani, (2016)

Katika mifano ya hapo juu maneno yaliyoandikwa kwa herufi mlazo yanabainisha virai nimino vyenye muundo wa kirai nomino uliohusisha kitenzi jina na kivumishi nayo ni ; *kuuka kwake, kucheza kwao, kwimba kwake, kwiba kwao na kucheka kwake.* Uchanganuzi wa kirai nomino cha kitenzi jina na kivumishi una muonekano ufuatao;

KN

N'

TJ

V

Kwimba

kwake

Aina hii ya virai nomino imejadiliwa na Hoekstra (2004) ambaye alibainisha muundo wa kipengele hicho katika lugha ya Kimacedonia na lugha nyingine za jamii ya Slavia kama vile Kirusi, Kichek, Kipolish, nk.

4.2.7 Kirai Nomino cha Muundo wa Nomino, Kivumishi na Kishazi Tegemezi

(N + V + Kish-teg)

Aina hii ya kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi inahusisha nomino, kivumishi na kishazi tegemezi kivumishi kama ilivyobainishwa hapa chini.

Jedwali Na. 4.7 Kirai Nomino cha Muundo wa Nomino, Kivumishi na Kishazi Tegemezi Kivumishi (N + V + Kish-teg - V)

Kimakunduchi	Kiswahili sanifu
<i>Mvulyana mwembamba mwakuja jana kauku leo</i>	Mvulana mwembamba aliyekuja jana kaondoka leo
<i>Kalamu nzuri nilokukwa zawadi ivunjiki</i>	Kalamu nzuri niliyopewa zawadi imevunjika
<i>Walimu wapya wanawake waajiriwa K/Samaki heya wahama</i>	walimu wapya wanawake waajiriwa K/Samaki wamehama
<i>Chakula kihibi kitamu kichovikwa jana mchana kisi</i>	chakula kidogo kitamu kilichopikwa jana mchana kimekwisha
<i>Kamusi kubwa iyonunulwa jana ibwa</i>	kamusi kubwa iliyonunuliwa jana imeibiwa

Chanzo: Uwandani, (2016)

Katika mifano ya hapo juu maneno yaliyoandikwa kwa herufi mlazo yanabainisha muundo wa kirai nomino uliyoundwa kwa nomino, kivumishi na kishazi tegemezi kivumishi nao ni; *Mvulyana mwembamba mwakuja jana, Kalamu nzuri nilokukwa zawadi, Walimu wapya wanawake waajiriwa K/Samaki, Chakula kihibi kitamu kichovikwa jana mchana na Kamusi kubwa iyonunulwa jana.*

Kijakazi (2012) katika uchunguzi wake wa lahaja ya Kitumbatu alibainisha virai nomino ambavyo vimeundwa kutokana na nomino, kivumishi na kishazi tegemezi kivumishi kwa mfano ; Kiatu kidugu kilichokwaga jana choneka [kiatu kidogo kilichopotea jana kimeonekana], maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi hiyo ni nomino, kivumishi na kishazi tegemezi kivumishi.

Uchanganuzi wa kirai nomino cha nomino, kivumishi na kishazi tegemezi kivumishi una muonekano ufaudao;

KN

N'

N V Kish- teg

Mvulyana mwembamba mwakuja jana

4.2.8 Kirai Nomino cha Muundo wa Kiwakilishi na Kivumishi (W+V)

Aina hii ya kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi inahusisha kirai nomino chenye mfuatano wa kiwakilishi na kivumishi kama iliyobainishwa hapa chini.

Jedwali Na. 4.8 Kirai Nomino cha Muundo wa Kiwakilishi na Kivumishi (W+V)

Kimakunduchi	Kiswahili sanifu
<i>Mie weka nngegoma kuvinua mizigo yopya</i>	Mimi peke yangu ningeweza kuinua mizigo yote
<i>Wao wenyewe wasababishi matatizo yopya</i>	Wao wenyewe wamesababisha matatizo yopya
<i>Nyuwe nyopya mchakwenda vuna</i>	Nyinyi nyote mtakwenda kuvuna
<i>Vyake vyopya vibwa</i>	Vyake vyote vimeibiwa
<i>Nvatia icho kidogo</i>	Nipatie hicho kidogo

Chanzo: Uwandani, (2016)

Katika mifano ya hapo juu maneno yaliyoandikwa kwa herufi mlazo yanaonesha virai nomino vya Kimakunduchi vinavyoweza kuundwa kwa kiwakilishi kufuatwa na kivumishi kwa mfano; *Mie weka, wao wenyuwe, nyuwe nyopya, vyake vyopya na nvatia icho kidogo.*

Uchanganuzi wa kirai nomino cha kitenzi jina una muonekano ufauatao;

KN

N'

W

V

Mie

weka

Kwa mujibu wa data zilizowasilishwa hapo juu muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi unatawaliwa na nomino ambayo huwa ni kiini cha kirai

nomino katika muundo wa kawaida vipashio vya kirai nomino huja baada ya nomino.

Katika miundo michache vipashio vya muundo wa kirai nomino vinatangulia vikifuatiwa na nomino.

Kama inavyooneshwa katika mifano ifuatayo;

Jedwali Na. 4.9 Vipashio vya Muundo wa Kirai Nomino

Kimakunduchi	Kiswahili sanifu
Kiya mwaka mwaka kogwa Makunduchi	Kila mwaka mwaka hukogwa Makunduchi
Kiya mwanakele mzuri	Kila mtoto mzuri
Baadhi ya samaki waozo	Baadhi ya samaki wameoza
Baadhi ya wanachuo wafeli	Baadhi ya wanachuo wamefeli

Chanzo : Uwandani, (2016)

4.3 Kuchanganua Utaratibu au Mpangilio wa Vipengele katika Kirai Nomino

Lengo la pili la utafiti huu linahusu kubainisha utaratibu au mpangilio wa vipengele vya muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi. Dhana hii inahusu virai nomino vyenye muundo unaohusisha nomino na vivumishi vingi (zaidi ya kimoja).

Data zifuatazo zinaonesha virai nomino mbalimbali vya lahaja ya Kimakunduchi inavyoundwa kutokana na nomino na vivumishi vingi na kishazi tegemezi (N+V+Kish-teg), kama data zinavyoonesha hapa chini.

4.3.1 Kirai Nomino chenye Nomino, Vivumishi na Kishazi Tegemezi (N+V+Kish-teg)

Aina hii ya kirai nomino kinahusisha nomino, kivumishi na kishazi tegemezi lengo likiwa kubainisha utaratibu wa mfuatano wa vipengele vya kirai nomino cha lahaja ya Kimakunduchi. Data zifuatazo zinaonesha mfuatano wa vivumishi katika kirai nomino;

**Jedwali 4.10 Kirai Nomino chenye Nomino, Vivumishi na Kishazi Tegemezi
(N+V+Kish-teg)**

1.

Kimakunduchi	wanakele	wadogo	wakorofí	waokuja jana	waga
Kiswahili sanifu	watoto	wadogo	wakorofí	waliokuja jana	wamepotea
M pangilio	N	V. umbile	V.tabia	V. Kish-teg	T

Chanzo : Uwandani, (2016)

2.

Kimakunduchi	kuku	wengi	weupe	waonunulwa leo	watoroko
Kiswahili sanifu	kuku	wengi	weupe	walionunuliwa leo	wametoro
M pangilio	N	V. idadi	V. rangi	V. kish- teg	T

Chanzo : Uwandani, (2016)

3.

Kimakunduchi	nguo	nyingi	nyeupe	mbovu	zizofuligwa	zibwa
Kiswahili sanifu	nguo	nyingi	nyeupe	mbovu	zilizofuliwa	zimeibiwa
M pangilio	N	V.idadi	V.rangi	V. hali	V.kish-teg	T

Chanzo : Uwandani, (2016)

4.

Kimakunduchi	mwanakele	mrefu	mweusi	maridadi	mwakuja jana	kafu
Kiswahili sanifu	mtoto	mrefu	mweusi	mtanashati	aliyekuja jana	amefariki
M pangilio	N	V.umbile	V. rangi	V.tabia	V. kish-teg	T

Chanzo : Uwandani, (2016)

5.

Kimakunduchi	samaki	wadogo	wadogo	watamu	waokaushwa	waligwa
K i s w a h i l i sanifu	samaki	wadogo	wadogo	watamu	waliokaushwa	wameliwa
M pangilio	N	V. umbile	V. umbile	V. ladha	V. kish- teg	T

Chanzo : Uwandani, (2016)

Vipengele vinavyojenga kirai nomino cha aina hii ni nomino ikifuatiwa na vivumishi na kishazi tegemezi. Kwa mujibu wa data zilizowasilishwa hapo juu inaonesha kwamba katika kirai nomino cha Kimakunduchi, vivumishi vyote hujitokeza mara tu baada ya nomino, vivumishi hivyo vinajitokeza katika mpangilio ufuatao;

N V.idadi + V. umbile + V. rangi + V. tabia/muonekano + V. ladha/hali.

Uchanganuzi wa kirai nomino cha nomino, kivumishi na kishazi tegemezi una muonekano ufuatao;

S

KN

KT

N'

Ts

T

N

KV

wadogo wadogo

samaki	watamu	waokaushwa	waligwa
--------	--------	------------	---------

4.3.2 Kirai Nomino cha Kiwakilishi na Vivumishi (W + V)

Aina hii ya kirai nomino kinaundwa na nomino, kiwakilishi na kivumishi. Uchanganuzi ufuatao unaonesha utaratibu wa mfuatano wa vipengele vinavyounda kirai nomino cha Kimakunduchi. Data zifuatazo zinaonesha mfuatano wa vivumishi katika kirai nomino ;

1. Jedwali 4.11 Kirai Nomino cha Kiwakilishi na Vivumishi (W + V)

Kimakunduchi	Mie	weka	nnegoma	kuvinua	mizigo	yopya
Kiswahili sanifu	Mimi	peke yangu	ningeweza	kuinua	mizigo	yote
Mpangilio	W	V. idadi	Ts	T	N	V. idadi

Chanzo : Uwandani, (2016)

2.

Kimakunduchi	vyake	vyopya	vizuri	vibwa
Kiswahili sanifu	vyake	vyote	vizuri	vimeibiwa
Mpangilio	W	V.idadi	V. muonekano	T

Chanzo : Uwandani, (2016)

3.

Kimakunduchi	nyuwe	nyopya	wadogo	wavivu	mchakwenda	vuna
Kiswahili sanifu	nyinyi	nyote	wadogo	wavivu	mtakwenda	kuvuna
Mpangilio	W	V.idadi	V. umbile	V. tabia	Ts	T

Chanzo : Uwandani, (2016)

Vipengele vinavyojenga kirai nomino cha aina hii huwa ni kiwakilishi kikifuatiwa na vivumishi. Kwa mujibu wa data vivumishi vinafuatia kiwakilishi ; navyo huwa katika mpangilio ufuatao :

W V. idadi + V. umbile + V. tabia. Hii ina maana kuwa kwa kawaida kiwakilishi hufuatiwa na vivumishi katika mpangilio ufuatao ; kivumishi cha idadi, hufuatiwa na kivumishi cha umbile, hufuatiwa na kivumishi cha tabia. Katika mifano iliyooneshwa hapo juu kirai nomino *mimi peke yangu* kimeundwa na mfuatano wa kiwakilishi na kivumishi cha idadi. Katika mfano mwengine *nyuwe nyopya wadogo* kirai nomino ambacho kimeundwa na mfuatano wa kiwakilishi na kivumishi cha idadi kikifuatiwa na kivumishi cha umbile.

Uchanganuzi wa kirai nomino cha kiwakilishi na kivumishi una muonekano ufuatao;

S

KN

KT

N'

Ts

KN

W

V

N

V

Wao wenyuwe wasababishi matatizo yopya

4.3.3 Kirai Nomino cha Nomino, Kitenzi Jina na Kivumishi (TJ+ V)

Kirai cha aina hii huundwa kutokana na kitenzi jina kinachofanya kazi ya nomino kikifuatiwa na kivumishi. Kama inavyooneshwa kwenye data zifuatazo hapo chini ;

1. Jedwali 4.12 Kirai Nomino cha Nomino, Kitenzi Jinan a Kivumishi (TJ+V)

Kimakunduchi	Kuimba	kwake	kuchaleta balaa
Kiswahili sanifu	kuimba	kwake	kutaleta balaa
M pangilio	TJ	V. kimilikishi	T

Chanzo : Uwandani, (2016)

Katika data iliyopo hapo juu inaonesha kwamba kitenzi jina kinafuatiwa na kivumishi kimilikishi.

2.

Kimakunduchi	kucheza	kwa Mussa	kuwachechesha wote
Kiswahili sanifu	kucheza	kwa Mussa	kunawachechesha wote
M pangilio	TJ	V – a unganifu	T

Chanzo : Uwandani, (2016)

Data za hapo juu zinaonesha kwamba kitenzi jina kikifuatiwa na kivumishi cha a-unganifu.

3.

Kimakunduchi	kucheka	kwao	kwingi	kuwafurahisha wote
Kiswahili sanifu	kucheka	kwao	kwingi	kunawafurahisha wote
M pangilio	TJ	V. kimilikishi	V.idadi	T

Chanzo : Uwandani, (2016)

Data hizo hapo juu zinaonesha kuwa kitenzi jina kikifuatiwa na kivumishi kimilikishi kikifuatiwa na kivumishi cha idadi.

Kwa mujibu wa data zilizowasilishwa hapo juu mpangilio wa vipengele vyta muundo wa kirai nomino cha kitenzi jina kinakuwa na utaratibu ufuatao; TJ V. kimilikishi/a-unganifu kikifuatiwa na kivumishi cha idadi.

Uchanganuzi wa kirai nomino cha nomino, kitenzi jina na kivumishi una muonekano ufuatao:

S

KN

KT

N'

T

KN

N

V

N'

Kucheza

kwake

kuchaleta

balaa

Kwa mujibu wa data zilizooneshwa hapo juu vipashio vyatia muundo wa virai nomino vinadhihirisha kuwa vipashio mbali mbali vinavyounda virai nomino vinafuata utaratibu maalumu wa mfuatano. Data zote zinaonesha kwamba kirai nomino cha Kimakunduchi kinatawaliwa na nomino (au kiwakilishi) ambayo aghlabu huwa ndicho kiini. Baada ya nomino hufuatia maneno ambayo ni vivumishi navyo vimegawika katika aina tatu nazo ni; vivumishi vikuu, vivumishi vyatia a-unganifu na vivumishi vyatia kishazi tegemezi. Vivumishi vikuu navyo hufuatana kwa utaratibu

maalumu; huanzia na vivumishi nya idadi, vikifuatiwa na vivumishi nya sifa (za msingi), vikifuatiwa na vivumishi nya sifa (za kawaida). Kama inavyooneshwa katika mchoro ufuatao;

Jadweli Na. 4.13 Muhtasari wa Vipengele nya Muundo wa Kirai Nomino cha Kimakunduchi.

Kirai nomino cha Kimakunduchi						
vivumishi awali	Nomino	Vivumishi tamati				
		Vivumishi vikuu			Vivumishi nya a-unganifu	Vivumishi nya k i s h a z i tegemezi
Baadhi ya	wanafunzi	v.idadi	v . s i f a msingi	v.sifa za kawaida	wa Tanzania	wa o k w e n d a China
Kiya	mwanakele			hodari		ayefaulu
	wasichana	wawili	weusi	warembo	wa bwana Mussa	waolegwa

Chanzo : Uwandani, (2016)

Uchanganuzi uliofanywa hapo juu unalingana na matokeo ya utafiti wa (Halliday, 1994 na Quirk na wenziwe, 1985) uliochunguza kutanuka kwa vikundi nomino waligundua kuwa kirai nomino kinaundwa na kibainishi ambacho hufuatiwa na kivumishi awali, neno kuu na kumalizia na kivumishi tamati. Kwa mfano ;

Jadweli Na. 4.14 Kutonuka kwa Vikundi Nomino

Kibainishi	Kivumishi awali	Neno kuu	Kivumishi tamati
several	new mystery	books	which we recently enjoyed

Chanzo : Halliday, (1994)

Katika uchunguzi huu imebainika kuwa katika lajaja ya Kimakunduchi kirai nomino kinatawaliwa na nomino (au kiwakilishi) ambayo aghlabu huwa ndicho kiini, na baada ya nomino hufuatia maneno ambayo ni vivumishi. Kwa upande wa Halliday na Quirk et al. (wameshatajwa) wamebainisha kuwa kirai nomino kinaundwa na

kibainishi ambacho hufuatiwa na kivumishi awali, neno kuu na kumalizia na kivumishi tamati.

Hivyo mpangilio wa vipengele vya muundo wa kirai nomino wa lahaja ya Kimakunduchi unatafautiana na ule wa Kiingereza.

4.4 Kubainisha Dhima za Kisarufi za Kirai Nomino katika Lahaja ya Kimakunduchi

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kubainisha dhima za kisarufi zinazotekelizwa na virai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi. Lengo likiwa kuonesha kazi zinazofanywa na virai hivyo katika miundo ya sentensi ya lahaja ya Kimakunduchi.

Dhima ya kisarufi ni nafasi ambayo neno au kikundi cha maneno hufanya kazi katika muundo wa sentensi, (Kim and Sells 2007). Kwa mujibu wa data zilizopatikana, kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi kina dhima zifuatazo za kisarufi ; dhima ya kiima ambayo ni neno, kirai au kishazi ambacho kinaonesha utendaji au kutendewa kulingana na kitendo kinachoelezwa na kitenzi, Hopper (1999), dhima ya pili ni yambwa tendwa (kipozi) ambayo ni neno linalotaja mtendwa katika muundo wa sentensi (Riro, 2012), dhima ya tatu ni kuwa yambwa tendewa (kitondo) inaelezea muhusika anayenufaika na tendo linaloelezwa na kitenzi (Riro, keshatajwa), dhima ya nne ni kuwa kijalizo cha kivumishi ni kijalizo ambacho kinajaliza kivumishi hasa cha ‘a’ unganifu. (Radford, (2004) na dhima ya tano ni kuwa kijalizo cha kihuishi ambacho ni neno linalotoa ufanuzi kuhusiana na kihuishi (Radford, keshatajwa). Data zifuatazo zinaonesha aina mbalimbali za dhima za kirai nomino cha lahaja ya Kimakunduchi.

4.4.1 Dhima ya Kubainisha Kiima katika Tungo

Dhima ya kwanza inayofanywa na kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi ni ile ya kubainisha kiima. Kiima ni neno, kirai au kishazi ambacho kinaonesha utendaji au kutendewa kulingana na kitendo kinachoelezwa na kitenzi (Hopper keshatajwa). Katika lugha ya Kiingereza dhana hii inajitokeza katika hali mbili. Kwanza kama kiima kinachowakilisha mtenda. Kwa mfano; the baby cried. [Mtoto alilia] maneno yaliyopigwa mstari katika sentensi hii ni kiima. Pili kama neno linaloelezea kiima, kwa mfano; My grandfather is a farmer. [Babu yangu ni mkulima] maneno yaliyopigwa mstari katika sentensi hiyo ni maneno yanayoelezea kiima. Katika kutekeleza dhima hii, kirai nomino hudhihirisha nafasi ya mtenda.

Data zifuatazo zinadhihirisha dhima ya kubainisha kiima katika tungo za lahaja ya Kimakunduchi;

Jadweli Na. 4.15 Dhima ya kubainisha Kiima katika Tungo

Kimakunduchi	Kiswahili sanifu
<i>Paka kanampiga panya</i>	Paka anampiga panya
<i>Katibu kamwandikii barua mhasibu</i>	Katibu amemuandikia barua mhasibu
<i>Kilimo cha kufwa na kupona kizingatigwa</i>	Kilimo cha kufa na kupona kimezingatiwa
<i>Yulya hodari kanapendwa</i>	Yule hodari anapendwa kweli
<i>Kwimba na kucheza kwake kuwapendezesha</i>	Kuimba na kucheza kwake kunawapendezesha

Chanzo : Uwandani, (2016)

Katika mifano iliyooneshwa hapo juu maneno yaliyoandikwa kwa hati za mlazo yanafanya kazi ya kiima, maneno haya hutawala na kuongoza maumbo mengine ya maneno yanayotokea baada ya kiima. Katika mifano hiyo hapo juu kiima kimeundwa

na aina mbalimbali za kirai nomino ambazo ni; nomino pekee, mfano *paka* nomino na kivumishi kwa mfano; *kwimba na kucheza kwake*, kiwakilishi na kivumishi kwa mfano; *yulya hodari*.

Uchanganuzi wa kubainisha kiima katika tungo una muonekano ufuatao;

S

KN

KT

N'

N

KH

T

cha

Kilimo

kufa na kupona

kizingatigwa

Kutokana na data zilizochambuliwa na mtafiti imebainika kuwa Kimakunduchi na Kiingereza vimefanana katika dhima ya kudhihirisha nafasi ya mtenda na kubainisha neno linaloelezea kiima.

4.4.2 Dhima ya kuwa Yambwa Tendwa (Kipozi)

Katika dhima ya yambwa tendwa (kipozi) kirai nomino kinafanya kazi ya kuwasilisha nafasi ya mtendwa katika sentensi. Dhana hii inafafanuliwa na (Riro,

keshatajwa) kwa kueleza kuwa yambwa tendwa ni jina la mtu au kitu kinachoathiriwa moja kwa moja na tendo linalotendwa na kiima. Hujibu swalii, “nini?” na “nani?” baada ya kitenzi. Data zifuatazo zinaoonesha namna kirai nomino cha Kimakunduchi kinavyodhihirisha dhima hiyo ya kisarufi.

Jadweli Na. 4.16 Dhima ya kuwa Yambwa Tendwa (Kipozi)

Kimakunduchi	Kiswahili sanifu
Juma kanasoma <i>kitabu</i>	Juma anasoma kitabu
Kevu kachukuu <i>mzigo</i>	Alikuwa amebeba mzigo
Askari waokwenda vitani wakwa <i>nishani</i>	Askari waliokwenda vitani wamepewa nishani
Nyoka avyoingia chumbani kauligwa <i>mpaka</i>	Nyoka alipoingia chumbani aliuawa na paka
Kijana ayepotea ameligwa <i>mfisi</i>	Kijana aliyepteota ameliwa na fisi
Juma kanalima <i>shamba lyetu</i>	Juma analima shamba letu

Chanzo : Uwandani, (2016)

Katika mifano iliyooneshwa hapo juu maneno yaliyoandikwa kwa hati za mlazo yanafanya kazi ya yambwa tendwa katika lahaja ya Kimakunduchi, nayo ni; *kitabu, mzigo, nishani, mpaka, mfisi na lyetu.*

Matokeo haya yanalingana na maelezo ya Kosur (2009) aliyechunguza yambwa tendwa katika Kiingereza na kuonyesha kuwa yambwa tendwa ni neno, kirai au kishazi kinachofuatia kitenzi kufafanua nani au nini kinachoathirika na kitendo kilichowakilishwa na kitenzi.

Uchanganuzi wa yambwa tendwa una muonekano ufuatao;

S

KN

KT

N'

T

KN

N

KV

N

V

Juma

kanalima

shamba

lyetu

4.4.3 Dhima ya kuwa Yambwa Tendewa (Kitondo)

Katika dhima ya yambwa tendewa (kitondo) kirai nomino kinafanyakazi ya kubainisha kitu au mtu ambaye anafaidi au kuathiriwa na kitendo kuitia kwa yambwa kipozi au mtendwa au yambiwa. (Riro, keshatajwa).

Data zifuatazo zinaonesha namna kirai nomino cha Kimakunduchi kinavyofanya dhima hiyo ya kisarufi;

Jadweli Na. 4.17 Dhima ya kuwa Yambwa Tendewa (Kitondo)

Kimakunduchi	Kiswahili sanifu
Jamila kawanunulii <i>wanakele</i> zawadi	Jamila kawanunulia watoto wake zawadi
Mkalimani kawatafsirii <i>waumini fungu kuu</i>	Mkalimani aliwatafsiria waumini fungu kuu
Siku zino <i>kulya</i> kunakalwa nyi wageni tu	Siku hizi kule kunakaliwa na wageni tu

Mwanafunzi kamjengee nyumba <i>mwalimu wake</i>	Mwanafunzi kamjengea nyumba mwalimu wake
Mie niandiki <i>kitabu kino</i> bila ya kushawishigwa	Mimi nimeandika kitabu hiki bila ya kushawishiwa

Chanzo : Uwandani, (2016)

Katika mifano iliyooneshwa hapo juu maneno yaliyoandikwa kwa hati za mlazo yanafanya kazi ya yambwa tendewa, maneno yenewe ni; *wanakele, fungu kuu, kulya, mwalimu wake na kitabu kino.*

Maelezo haya yanalingana na uchunguzi wa Matthews (1981) aliyechunguza yambwa tendewa katika Kiingereza na kuonyesha kuwa yambwa tendewa ni maneno yanayoelezea kitendo kimefanywa kwa niaba ya nani au nini. Mifano ya hapo juu inachanganuliwa kwa njia ya matawi kama ifuatavyo:

- i. Jamila kwanunulii wanakele zawadi.

S

KN

KT

N'

T

KN

N

KV

N

V

Jamila

kawanunulii

wanakele

zawadi

4.4.4 Dhima ya kuwa Kijalizo cha Kiima

Kijalizo cha kiima ni neno au kikundi cha maneno ambacho huelezea au kufafanua zaidi taarifa za kiima, (Radford keshatajwa) Data zilizowasilishwa hapa chini zinaonesha namna kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi kinavyofanya kazi ya kijalizo cha kiima:

Jadweli Na. 4.18 Dhima ya kuwa Kijalizo cha Kiima

Kimakunduchi	Kiswahili sanifu
Jeshi ni <i>mchapakazi</i>	mwanajeshi ni mchapakazi
Kami si <i>mwalimu mzuri</i>	Kami si mwalimu mzuri
Mwanakele kanaoneka <i>mtundu</i>	mtoto anaonekana mtundu
Mjomba kevu <i>mgeni yetu leo</i>	mjomba alikuwa mgeni wetu leo
Wanafunzi wangali <i>wakorofi</i>	wanafunzi bado wakorofi

Chanzo : Uwandani, (2016)

Katika mifano iliyooneshwaa hapo juu maneno yaliyo katika hati mlazo yanawasilisha virai nomino vya Kimakunduchi vinavyofanyakazi ya kuwa kijalizo cha kiima navyo ni; *mchapakazi, mwalimu mzuri, mtundu, mgeni yetu leo na wakorofi.*

Matokeo haya yanalingana na maelezo ya Kosur (2009) ambaye alieleza kuwa kazi moja wapo ya kirai nomino katika lugha ya Kiingereza ni kuwa kijalizo cha kiima. Uchanganuzi ufuatao wa sentensi unaonesha namna kirai nomino cha Kimakunduchi kinavyofanyakazi kama kijalizo cha kiima.

S

KN

KT

N'

t

KN

N'

Jeshi

ni

mchapakazi

Katika uchanganuzi ulioelezwa hapo juu, kirai nomino *mchapakazi* kinafanya kazi ya kijalizo cha kiima kwa sababu kinafafanua zaidi kuhusu kiima *jeshi*.

4.4.5 Dhima ya kuwa Kijalizo cha Kivumishi

Kijalizo cha kivumishi ni kijalizo ambacho kinajaliza kivumishi hasa cha ‘a’ unganifu. (Radford, keshatajwa)

Data zilizowasilishwa hapa chini zinaonesha kwamba katika lahaja ya Kimakunduchi kuna muundo wa kirai nomino chenye mfuatano wa nomino na kijalizo cha kivumishi cha a-unganifu

Data zinadhihirisha hilo katika sentensi zifuatazo:

Jadweli Na. 4.19 Dhima ya kuwa Kijalizo cha Kivumishi

Kimakunduchi	Kiswahili sanifu
Uongo wa <i>wanasiasa nchini</i> umekoneka	Uongo wa wanasiasa nchini umedhiihirika
Kiatu <i>cha dada</i> chaga	Kiatu cha dada kimepotea
Jeshi <i>lya mgambo</i> limefika	jeshi la mgambo limewasili
Maji <i>ya moto</i> yamwagiki	maji ya moto yamemwagika
Nguo <i>za usufi</i> zinunulwa	Nguo za sufi zimenunuliwa

Chanzo : Uwandani, (2016)

Katika mifano iliyooneshwa hapo juu maneno yaliyo katika hati mlazo yanawasilisha virai nomino vya Kimakunduchi vinavyofanyakazi ya kuwa kijalizo cha kivumishi cha a-unganifu navyo ni : *wanasiasa nchini, cha dada, lya mgambo, na za usufi*.

Matokeo haya yanalingana na maelezo ya Kim na Sells (2007) ambaye alieleza kuwa kazi moja wapo ya kirai nomino katika lugha ya Kiingereza ni kuwa kijalizo cha kivumishi.

Uchanganuzi ufuatao wa sentensi unaonesha namna kirai nomino cha Kimakunduchi kinavyofanyakazi kama kijalizo cha kivumishi.

	S	
KN		KT
N'		T
N	KV	
Uongo	wanasasia	umekonekana
	wa	
	nchini	

Katika uchanganuzi ulioelezwa hapo juu kirai kivumishi *wa wanasasia nchini* ni kijalizo cha kivumishi kwa sababu kinafanyakazi ya kuvumisha kirai nomino.

4.4.6 Dhima ya kuwa Kijalizo cha Kihuishi

Dhima nyingine ya kisarufi kirai nomino ni ile ya kuwa Kijalizo cha kihuishi. Katika dhima hii, kirai nomino hufanya kazi ya kutoa ufanuzi kuhusiana na kihuishi.

Data zilizokusanywa zinaonesha kwamba katika lahaja ya Kimakunduchi kuna muundo wa kirai nomino chenye mfuatano wa nomino na kijalizo cha kihuishi.

Data zinadhahirisha hilo katika sentensi zifuatazo:

Jadweli Na. 4.20 Dhima ya kuwa Kijalizo cha Kihuishi

Kimakunduchi	Kiswahili sanifu.
Paka kalala <i>juu ya kitanda changu.</i>	paka amelala juu ya kitanda changu.
Panya kaviti <i>chini ya kabati lyangu.</i>	panya kapita chini ya kabati langu
Mwanafunzi kapigwa <i>kwa sababu ya makosa yake.</i>	mwanafunzi alipigwa kwa sababu ya makosa yake.
Ali kavata pesa nyingi <i>zaidi ya nduguze.</i>	Ali amepata pesa nyingi zaidi ya nduguze

Chanzo : Uwandani, (2016)

Katika mifano iliyooneshwa hapo juu maneno yaliyo katika hati mlazo yanawasilisha virai nomino vya Kimakunduchi vinavyofanyakazi ya kuwa kijalizo cha kihuishi nayo ni ; *kitanda changu, kabati lyangu, makosa yake, na nduguze.*

Pia dhana hii inakubaliana na Rodney (1984) ambaye alieleza kuwa kazi moja wapo ya kirai nomino katika lugha ya Kiingereza ni kuwa kijalizo cha kihuishi.
Uchanganuzi wa kijalizo cha kihuishi una muonekano ufuatao ;

S

KN

KT

T

KH

H'

KN'

N'

N

V

kwa

Mwanafunzi kapigwa kwa sababu ya makosa yake

Katika uchanganuzi ulioelezwa hapo juu kirai nomino *makosa yake* ni kijalizo cha kihusishi kwa sababu kinafanyakazi ya kukamilisha kihusishi *kwa sababu ya*.

Katika sura hii tumbainisha muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi ambapo ushahidi wa data umeonesha kuwa kirai nomino kina miundo mbalimbali ifuatayo; nomino moja pekee, nomino na kivumishi, wakati mwengine hujengwa kwa kiwakilishi na kivumishi, au kiwakilishi pekee. Vilevile kinaweza kujengwa kwa nomino na kishazi tegemezi, kitenzi jina na kivumishi, kitenzi jina na nomino, na kivumishi na kishazi tegemezi yumishi.

Sehemu hii pia imechambua utaratibu au mpangilio wa vipengele vya kirai ushahidi wa data umeonesha kwamba kama ilivyo katika lugha nyengine kirai nomino cha Kimakunduchi kinatawaliwa na nomino ambayo aghlabu huwa ndicho kiini.

M pangilio wa vipengele vya kirai nomino cha Kimakunduchi huwatawaliwa na nomino ambayo hufuatiwa na maneno yanayoelezea sifa za nomino (vivumishi) ambayo yamegawika katika aina tatu nazo ni; vivumishi vikuu, vivumishi vya a-unganifu na vivumishi vya kishazi tegemezi. Vivumishi vikuu navyo hufuatana kwa utaratibu maalumu; huanzia na vivumishi vya idadi, vivumishi vya sifa (ya msingi), vivumishi vya sifa za kawaida. Vilevile tumechambua dhima za kirai nomino cha Kimakunduchi na kuonesha kinaweza kufanyakazi kama yambwa

tendwa, yambwa tendewa, kijalizo cha kiima, kijalizo cha kihuishi na kijalizo cha kivumishi.

Kwa mujibu wa data zilizowasilishwa hapo juu na uchambuzi uliofanywa, matokeo yafuatayo yamebainika kuhusu muundo wa kirai nomino cha Kimakunduchi; kwanza kuhusu vipengele vya kumuundo, imebainika kuwa Kimakunduchi kina virai vya aina zifuatazo; kirai cha nomino moja pekee, nomino na kivumishi, kiwakilishi na kivumishi, kiwakilishi pekee, nomino na kishazi tegemezi, kitenzi jina na kivumishi, kitenzi jina pekee na nomino, kivumishi na kishazi tegemezi vumishi.

Kuhusu mpangilio wa aina za maneno katika kirai nomino, ushahidi wa data umeonesha kuwa kirai nomino cha Kimakunduchi kinatawaliwa na nomino ambayo aghlabu huwa ndicho kiini. Baada ya nomino hufuatia maneno ambayo ni vivumishi navyo vimegawika katika aina tatu nazo ni; vivumishi vikuu, vivumishi vya a-unganifu na vivumishi vya kishazi tegemezi. Vivumishi vikuu navyo hufuatana kwa utaratibu maalumu; huanzia na vivumishi vya idadi, vivumishi vya sifa (ya msingi), vivumishi vya sifa za kawaida.

Kuhusu dhima za kisarufi ambazo zinafanywa na virai nomino imebainika kuwa, kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi kina dhima zifuatazo za kisarufi; dhima ya kwanza ni kubainisha kiima katika tungo; kiima ni neno, kirai au kishazi ambacho kinaonesha utendaji au kutendewa kulingana na kitendo kinachoelezwa na kitenzi (Hopper 1999), dhima ya pili ni yambwa tendwa (kipozi) dhana hii inafafanuliwa na

(Riro 2012) kwa kueleza kuwa yambwa tendwa ni jina la mtu au kitu kinachoathiriwa moja kwa moja na tendo linalotendwa na kiima, dhima ya tatu ni kuwa yambwa tendewa (kitondo) ni kirai nomino ambacho kinafanyakazi ya kubainisha kitu au mtu ambaye anafaidi au kuathiriwa na kitendo kuitia kwa yambwa kipozi au mtendwa au yambiwa (Riro, keshatajwa), dhima ya nne ni kuwa kijalizo cha kiima ni neno au kikundi cha maneno ambacho huelezea au kufafanua zaidi taarifa za kiima, (Radford keshatajwa), dhima ya tano ni kuwa kijalizo cha kivumishi ni kijalizo ambacho kinajaliza kivumishi hasa cha ‘a’ unganifu (Radford, keshatajwa) na dhima ya sita ni kuwa kijalizo cha kihuishi ni kijalizo ambacho kirai nomino hufanya kazi ya kutoa ufanuzi kuhusiana na kihuishi (Radford, keshatajwa).

4.5 Hitimisho

Sura hii imewasilisha na kuchambua data zilizokusanywa katika utafiti huu. Maeleo yameanza na utangulizi wa sura na kufuatiwa na ubainishaji wa miundo mbalimbali ya kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi kisha imechanganua utaratibu au mpangilio wa vipengele katika kirai nomino na kuelezea mpangilio wa vipengele katika kirai nomino. Vilevile ilielezea dhima za kisarufi za kirai nomino na kumalizia na muhtasari wa matokeo ya utafiti pamoja na hitimisho la sura.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

5.1 Utangulizi

Hii ni sura ya mwisho ya ripoti ya utafiti uliochunguza muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi. Katika sura hii mtafiti ameangalia muhtasari wa utafiti huu, hitimisho juu ya data iliyopatikana katika utafiti huu, na mapendekezo ya utafiti. Malengo mahsusini ya utafiti huu yalikuwa ni kubainisha vipengele vya muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi; kuelezea mpangilio au utaratibu wa vipengele vya muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi pamoja na; kujadili dhima za kisarufi za kirai nomino cha lahaja ya Kimakunduchi.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi. Malengo mahsusini yalikuwa matatu, ambayo ni; kubainisha vipengele vya muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi; kuelezea utaratibu au mpangilio wa vipengele vya muundo wa kirai nomino; na kujadili dhima za kisarufi za kirai nomino cha lahaja ya Kimakunduchi. Muundo wa utafiti uliotumika ulikuwa wa kimaelezo katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Pia utafiti huu ulifanyika katika shehia tatu nazo ni shehia ya Kiongoni, shehia ya Nganani na shehia ya Mzuri. Walengwa wa utafiti walikuwa ni wakaazi wote wa Makunduchi ambao ni watumiaji wa asili wa lahaja hii kati yao waliteuliwa walengwa (60) kama sampuli ya washiriki

wa utafiti huu, thelathini (30) wanawake na thelathini (30) ni wanaume, wazee na vijana wenye umri wa kati ya miaka 30 na 70.

Data zimekusanya kwa kutumia mbinu ya hojaji na uchunguzi makini kupitia shughuli za kijamii kwa mfano mwaka kogwa, sherehe za harusi, maziko na kadhalika. Data zilichanganuliwa kwa kutumia mkabala stahilifu ambao ni ule unaotumia maelezo katika kuchanganua data. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Sarufi miundo virai na dhana yake maarufu ya mahusiano ndani ya kirai inayojulikana kama eksibaa. Maadili ya kiutafiti yalizingatiwa, ambayo ni pamoja na kupata kibali au ridhaa ya kufanya utafiti, kujadiliana na kundi lengwa juu ya utafiti wake ili kuepusha matatizo, kuwa wazi katika utafiti wake ili kupata taarifa kwa urahisi, kulinda haki za watu vilevile faragha na usikivu, kuheshimu usiri wa wale waliohusika katika uchunguzi pia kuweka siri zao na utambulisho wao, kuwa muaminifu na muadilifu katika kazi yake, kuelewa sheria za nchi kuhusiana na utafiti n.k.

5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umebainisha matokeo yafuatayo ; kwanza, muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi una vipengele vinane kama ifuatavyo ; nomino moja pekee, nomino na kivumishi, kiwakilishi na kivumishi, kiwakilishi pekee, nomino na kishazi tegemezi, kitenzi jina na kivumishi, kitenzi jina pekee na nomino, kivumishi na kishazi tegemezi vumishi.

Pili, vipengele vya kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi vipo katika mpangilio ufuatao ; kirai nomino kinatawaliwa na nomino ambayo aghlabu huwa ndicho kiini. Baada ya nomino hufuatia maneno ambayo ni vivumishi navyo vimegawika katika aina tatu zifuatazo; vivumishi vikuu, vivumishi vya a-unganifu na vivumishi vya kishazi tegemezi. Vivumishi vikuu navyo hufuatana kwa utaratibu maalumu; huanzia na vivumishi vya idadi, vivumishi vya sifa (ya msingi), vivumishi vya sifa za kawaida.

Tatu, dhima za kisarufi ambazo zinafanywa na virai nomino imebainika kuwa, kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi kina dhima zifuatazo za kisarufi; dhima ya kwanza ni kubainisha kiima katika tungo, dhima ya pili ni kuwa yambwa tendwa (kipozi), dhima ya tatu ni kuwa yambwa tendewa (kitondo), dhima ya nne ni kuwa kijalizo cha kiima, dhima ya tano ni kuwa kijalizo cha kivumishi na dhima ya sita ni kuwa kijalizo cha kihuishi.

5.4 Mapendekezo

Baada ya kufanya utafiti huu pamoja na matokeo yaliyopatikana, mapendekezo yafuatayo yanatolewa. Mapendekezo yamegawanywa katika makundi mawili; mapendekezo ya jumla na mapendekezo ya tafiti fuatishi, kama inavyooneshwa hapa chini;

i.1.1 Mapendekezo ya Jumla

Ili kukuza lugha ya Kiswahili mtafiti anashauri yafuatayo:

Kwanza, serikali na watendaji wa Idara za Kiswahili waunde chombo cha ukuzaji na uendelezaji wa lahaja za Kiswahili.

Pili, serikali ishajihishe wataalamu wa lugha kuzifanyia utafiti lahaja za Kiswahili na kuziandikia sarufi yake kwa lengo la kukuza na kukiendeleza Kiswahili. Mtazamo huu utaweza kukuza soko la ushindani la kuzitangaza na kuziendeleza lahaja za Kiswahili na kuweza kuinufaisha serikali na waswahili kwa ujumla katika kukuza uchumi wa nchi na wananchi.

Tatu, serikali na vyombo vya kukuza Kiswahili izitumie tafiti zilizofanywa kwa lengo la kuendeleza maendeleo ya jamii.

5.4.2 Tafiti Fuatishi

Utafiti huu umechunguza “Muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi” Mtafiti anapendekeza maeneo yafuatayo yafanyiwe utafiti wa kina:

Kwanza, baada ya utafiti huu kuonyesha muundo na dhima za kisarufi za kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi, ingefaa tafiti fuatishi zifanywe ili kuchunguza muundo wa kirai kitenzi.

Pili, kutokana na uwezekano kuwa baadhi ya lahaja za Kiswahili zinaweza kuwa zimeathiriwa na lugha nyengine ingefaa tafiti fuatishi zifanywe ili

kulinganisha muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi na lahaja nyengine za Kiswahili, kama vile Kipemba.

Tatu, kutohana na lahaja nyingi za Kiswahili kuathiriwa na Kiswahili sanifu, ingefaa tafiti fuatishi zifanywe ili kuchunguza athari ya Kiswahili sanifu katika lahaja nyengine za Kiswahili.

5.5 Hitimisho

Sura hii imehitimisha utafiti unaohusu “Muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi”. Sehemu ya kwanza imeeleza muhtasari wa utafiti mzima. Sehemu ya pili imetoa muhtasari wa matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu. Sehemu ya tatu imeeleza mapendekezo ya utafiti kuhusu muundo wa kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi na sehemu ya nne imeelezea hitimisho.

MAREJEO

- Akmajian, A. Demers, R. A.na Farmer, A. K. (2007). *Linguistics: An Introduction to Language And Communication*, (Toleo la tano) Cambridge U.S.A: MIT Press.
- Ashton, E. O. (1944). *Swahili Grammar: Including Innotation*. London: Longmans
- Culicover, P. (1976). *Syntax* New York: Academic Press.
- Fromkin, V.A. (2000). *Linguistics: An Introduction to Linguistics Theory*. Blackwell Publishers Inc. Malden, USA: Massachussetts.
- Halliday, M. (1994) *Introduction Grammar*. (Toleo la pili) London: Edward Arnold.
- Hoekstra, T. (2004). *Arguments and structure*. Berlin: Mouton de Gruyter.
- Hopper, P. (1999). *A short course in grammar*. New York: W. W. Norton & Company.
- Huddleston, R. (1984). *Introduction to the Grammar of English*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Hudson, G. (2000). *Essentials Introductory Linguistics*, U.S.A: Blackwell Publishing Ltd.
- Issah, S. (2013). The structure of the Dagbani simple noun phrase. *South African Journal of African Languages*, (Disemba 2014), 37–41.
- Kadege, M. (2009). English for Tanzania Secondary Schools. Forms 1, 2.3 and 4, Dar es salaam: ECOM Graphics Publishers
- Khamis, A. (2009) Stadi za Lughya ya Kiswahili, SARUFI. Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam : TUKI.

- Kijakazi, M. (2012). *Miundo ya Virai Nomino katika Lahaja ya Kitumbatu*. Chuo Kikuu cha Dar es salaam : Dar es salaam University Press.
- Kim, J. na Sells, P (2007) *English Syntax and Introduction*. Chicago : University of Chicago Press.
- Kitchin, R. na Tale, N. (2000). *Conducting Research into Human Geography: Theory, Methodology and Practice*, UK: Pearson Education Limited.
- Kombo, D. and Tromp, D. (2006). *Proposal and Thesis Writing; Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Kosur, H. (2009) *The Grammatical Noun Phrase Modifier in English* www.usingenglish.com.glossary/noun-phrase.htm (Imesomwa tarehe 6 Nov, 2016).
- Kothar, C.R. (2004). *Research Methodology, Methods and Techniques* (Toleo la pili), New Delhi; New Age International (P) Limited Publishers.
- Kothar, C.R. (2009). *Research Methodology. Methods and Techniques* (Toleo la pili), New Delhi; New Age International (P) Limited Publishers.
- Leffel, K. na Bouchard, D. (1991). *Views on Phrase Structure* Kluwer Academic Publishers, Dordrecht, The Netherlands
- Longhorn. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn.
- Lusekelo, A. (2009). *The Structure of the Nyakyusa Noun Phrase*, <http://www.njas.helsinki.fi/pdf-files/voll8nu4/lusekelo> 26 Machi, 2011.
- Magashi, S. (2008). *Kisukuma Noun Phrase Structure*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Dar es salaam University Press.

- Masebo, J. na Nyangwine. (2007). *Nadharia ya Lugha Kiswahili 1 Kidato cha 5&6*, Dar-es-Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.
- Massamba na wenzake. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. TUKI, Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam.
- Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Matei, A. (2008) *Sarufi Kamili ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix.
- Matthews, P. (1981) *Syntax*. Cambridge, UK : Cambridge University Press.
- Mbaabu, I. (1985). *Sarufi ya Kiswahili*. Longman Kenya: Nairobi.
- Mdee, J.S. (1999). *Sarufi ya Kiswahili Sekondari na Vyuo*, Dar es Salaam : Dar es Salaam University Press.
- Mluya, E.E. (2011). *A Simplified Guide to Research Proposal and Report Writing for Institution of Higher Learning*. Dar-es-salaam: Ecumenical Gathering Publishers.
- Mtallo, G. (2015). *Analysis of Kiuru Noun Phrase*. Dodoma: College of Business Education (CBE)
- Ndomba, R. (2006). *Samategi Noun Phrase Structure*. Chuo Kikuu Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Neekemiah, N. R. (2010). *Noun Phrase Structure in Kihangaza*. Chuo Kikuu cha Dar es salaam : Dar es Salaam University Press.
- Oxford, R. (2011). *Kiswahili Kidato cha 5-6*. Dar es Salaam: Oxford University Press Tanzania Ltd.

- Prewitt, E.C. (1980). *Introductory Research Methodology*. East Africa Applications Occasional Papers No. 10. Institute for Development Studies, University.
- Quirk R, Leech G, and Svartvik J. (1985). *A Comprehensive Grammar of the English Language*. London: Longman
- Radford, A. (1997). *Transformational Grammar*. Great Britain: Cambridge University Press.
- Radford, A. (2004). *English Syntax: An introduction*. Great Britain: Cambridge University Press.
- Rijkhoff, J. (2002). *The Noun Phrase*, London: Oxford University Press.
- Riro, S. Matinde. (2012). *Dafina ya Lugha. Isimu na Nadharia*. Dar es Salaam: Serengeti Educational Publishers.
- Rugemalira, J. (2005). *A Grammar of Runyambo*. Dar es Salaam: DUP.
- Rugemalira, J. (2007). *The Structue of Bantu Noun Phrase*. SOAS Working Papers in Linguistics Vol. 15: (135 – 18), Dar es salaam: Dar es Salaam University Press.
- Shaw S, Petchey R, Chapman J, Abbott S. (2009). "A double- edged upanga? <https://sw.wikipedia.org/wiki/UtafitiwamaadiliJumpup> (Imesomwa 7 Juni, 2016)
- Sign, K. (2007). *Quantitative Social Research Methods*; India: SAGE Publication
- TUKI. (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu ya Lugha*. Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam: TUKI.

- Wabwire, V. (2013). *The Structure and Function of Olukhayo Noun Phrase: An X-Bar Perspective*. Kenya: Kenyatta University Press.
- Walliman, N. (2011). *Research Methods: The Basic*, London & New York: Routledge Taylor & Francis Group.
- Wozna and Wilson. (2005). *Seimat Grammar Essentials; Data Papers on Papua New Guinea*. Guinea Language, Vol 48.

www.iiste.org > Home > Vol 5, No 14 (2015) > inusah.www.tandfonline.com

VIAMBATANISHO

KIAMBATANISHO A. Hojaji kwa wakaazi wa Makunduchi

Mimi ninaitwa Asha Iddi Bavuai ni mwanafunzi wa shahada ya Uzamili (M. A. Kiswahili) katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Ninafanya utafiti kuhusu Muundo wa Kirai Nomino katika Lahaja ya Kimakunduchi ili kuweza kukamilisha program ya shahada hii. Hojaji hii imeandalowiwa kwa makusudi ya kupata taarifa zitakazokamilisha utafiti huu. Hivyo ninaomba ushirikiano wako katika kukamilisha malengo ya utafiti huu.

Tafadhali unaombwa kujibu maswali yafuatayo kwa mujibu wa uelewa wako na kwa usahihi ili usaidie kutoa matokeo yakinifu yatakayochangia maendeleo ya Kiswahili. Majibu yatakayotolewa yatakuwa ni siri ya mtafiti na hayatatumika kwa malengo mengine yoyote zaidi ya utafiti huu.

SEHEMU YA KWANZA: MAELEZO BINAFSI.

- | | | |
|--|---------|---------|
| 1. JINSIA: | mke | mme |
| | | |
| 2. UMRI : 30 – 39 | 40 – 59 | 60 – 70 |
| | | |
| 3. KIWANGO CHAKO CHA ELIMU | | |
| 4. KIJIJI UNACHOISHI | | |
| 5. MIAKA MINGAPI UMEISHI KATIKA KIJIJI HICHO | | |

SEHEMU YA PILI: MAELEZO KUHUSU VIRAI NOMINO.

Katika maswali yafuatayo badilisha sentensi zifuatazo kuwa katika lahaja ya Kimakunduchi.

1. Mbuzi aliyechinjwa juzi alikuwa anaumwa.
-

2. Mwalimu aliyeondoka mwaka jana amerudi tena.
-

3. Baba alipoondoka jana nilikuwa nimelala.
-

4. Kijana hodari ameshinda.
-

5. Mtoto mzuri anaogopa.
-

6. Mimi peke yangu ningeweza kuinua mzigo wote.
-

7. Wao wenyewe wamesababisha matatizo yote.
-

8. Ninyi nyote mtaenda kuvuna.
-

9. Vyake vyote vimeibiwa.
-

10. Kuondoka kwake kumewafurahisha wengi.

.....

11. Mtoto mdogo mkorofsi amepotea.

.....

12. Mvulana mwembamba aliyejua jana ameondoka.

.....

13. Hili jino limeoza.

.....

14. Yule mtu alipita hapa jana.

.....

15. Wale wanachuo wamegoma kufanya jaribio.

.....

16. Nipatie hicho kidogo.

.....

17. Msichana aliyeiba nguo amekamatwa.

.....

18. Hao watoto wana matatizo.

.....

19. Hili kubwa litamfaa.

.....

20. Hicho chumba kitapangishwa.

.....

21. Chui anakula.

.....
22. Jiwe limedondoka.

.....
23. Ujeuri na kiburi ulikuwa kwao.

.....
24. Papa, nguru na pweza wamepatikana kwa wingi.

.....
25. Paka na panya wanafukuzana.

.....
26. Masika imeshamiri.

.....
27. Sisi ni wanafunzi.

.....
28. Nyinyi mtakuja kesho.

.....
29. Wewe hupendi hisabu.

.....
30. Mimi peke yangu ningeweza kuinua mizigo yote.

.....
31. Wao wenyewe wamesababisha matatizo yote.

.....
32. Vyake vyote vimeibiwa.

33. Kucheza kwake kutaleta balaa.

.....

34. Kalamu nzuri niliyozawadiwa imevunjika.

.....

35. Kamusi kubwa iliyonunuliwa jana imeibiwa.

.....

36. Samaki wadogo wadogo watamu.

.....

37. Mtoto mdogo mkorofsi amepotea.

.....

38. Yule mtu alipita hapa jana.

.....

39. Paka amelala juu ya kitanda.

.....

40. Huyu ni mtu wa hasira nyingi.

.....

41. Kiatu cha dada kimepotea.

.....

42. Jeshi la mgambo limewasili.

.....

43. Mjomba alikuwa mgeni wetu leo.

.....

44. Wanafunzi bado wakorofsi.

.....

45. Kama una maelezo ya ziada andika hapa.

.....

.....

AHSANTE KWA USHIRIKIANO WAKO.